**Wapendekeza** kufutwa viti maalumu vya ubunge, udiwani
UKURASA 3

**Mbeba** mkaa afariki dunia purukushani na polisi, TFS
UKURASA 5

**MAISHA YALIVYO**
Mume aenda masomoni, kurudi mkewe mjamzito
UKURASA 11




UKURASA 9

Jumapili Machi 10, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581611
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Simulizi mwanachuo aliyeolewa na nyapala

**WALIKUTANA** gerezani akisubiri kunyongwa hadi kufa ... *Endelea ukurasa wa 4*



Luteni Kanali, Patrick Sawala    Daniel Chongolo    Paul Chacha.

**Paul Chacha**
Mkuu mpya wa Mkoa wa Tabora

**Daniel Chongolo**
Mkuu mpya wa mkoa wa Songwe

**Luteni Kanali Patrick Sawala**
Mkuu mpya wa Mkoa wa Mtwara

**Waziri Kindamba**
Mkurugenzi Mkuu mpya wa Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART),



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akikagua majiko yanayotumia nishati ya gesi na umeme, alipotembelea maonyesho katika Kongamano la Wanawake la Nishati Safi ya Kupikia, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Waziri Kindamba

## Maoni tofauti wadau pangua pangua ya wateule wa Rais

**KINDAMBA** atwishwa zigo UDART... *Ukurasa wa 2*

## Samia abeba rasmi ajenda nishati safi ya kupikia



UKURASA 3

UKURASA WA 7

### TAYARI TUNAUMWA KIUCHUMI, MSITUROGE KISIASA

SI siri kwamba idadi kubwa ya Watanzania tunapitia kipindi...

UKURASA WA 24

### YANGA : HARUFU YA UBINGWA INANUKIA

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya wenyeji Namungo FC, Kocha...

**MICHEZO** HATIMA SAKATA LA DUBE J'TANO, ATAJWA YANGA UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kindamba atwishwa zigo UDART

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Kindamba, ambaye kabla ya mabadiliko yaliyofanywa jana na Rais Samia Suluhu Hassan, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mabasi Yaendayo kasi Dar es Salaam (UDART).

Kindamba, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, anachukua nafasi ya Gilliard Ngewe ambaye atapangiwa kazi nyingine.

Kutokana na uteuzi huo, Kindamba ametwishwa zigo ambalo limeonekana kuwa zito kutokana na matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza ndani ya kampuni hiyo ambayo serikali ina idadi kubwa ya umiliki wa hisa.

UDART, tangu kuanza kazi mwaka 2016, imekuwa ikilalamikiwa kwa madai ya kushindwa kutimiza wajibu wake kutokana na mambo mbalimbali yakiwamo usimamizi mbovu kutoka kwa watendaji.

Sababu nyingine ni idadi ndogo ya mabasi ya kubeba abiria kulinganisha na mahitaji halisi huku zikiwapo taarifa kwamba mabasi mengi yamechakaa ama kutokana na kuharibika kwenye yadi yake iliyoko jangwani, Dar es Salaam kwa sababu ya mvua au kutelekezwa, hivyo kutokufanya kazi kabisa. Hali hiyo imefanya baadhi ya mabasi hayo kutotengenezeka, hivyo kuwa hasara kwa wamiliki.

Kwa mujibu wa uchunguzi ambao uliwahi kufanywa pia na gazeti hili, ilibainika kwamba kumekuwa na upotevu wa fedha kutokana na baadhi ya mashine za kielektroniki za kukatia tiketi za abiria kuharibika. Hatua hiyo ilisababisha baadhi ya watumishi wasio waminifu kutumia mwanya huo na kukwapua mamilioni ya shilingi.

**RIPOTI YA CAG**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya miaka minne iliyopita ambayo ilikagua utendaji wa kampuni hiyo, iligundua kuwapo upungufu wa mabasi 165 hali inayosababisha kushindwa kukidhi mahitaji ya abiria kwa siku.

Katika awamu ya kwanza ya mradi huo ulioanza Mei 10, 2016 magari yalipaswa kuagizwa ni 306 lakini ni 165 pekee ndiyo yaliyoingizwa hivyo kuwa na upungufu mkubwa.

Kutokana na upungufu huo, CAG alisema mabasi yaliyopo yamekuwa yanajaa kupita uwezo, hivyo kusababisha uchakavu na uharibifu wa haraka. Pia alisema hali hiyo imesababisha ucheleweshaji wa usafiri kwa wananchi.

CAG pia alisema UDART ilikuwa ikijiendesha kwa hasara, akibainisha kuwa katika muda huo kampuni ilipata hasara ya Sh. bilioni 6.78. Alibainisha kuwa mapato ya kampuni yalikuwa Sh. bilioni 19.78 wakati matumizi yalikuwa Sh. bilioni 26.57.

Sambamba na hayo, CAG pia alibaini kuwapo kwa matumizi yenye shaka baada ya kugundua kuwa tarifa zilionyesha kuwa matumizi ya mafuta yalikuwa Sh. bilioni 6.02 wakati vitabu vikionyesha yalikuwa Sh. bilioni 4.79.

Aidha, kutokana na hasara hiyo, serikali kupitia Msajili wa Hazina, haijawahi kupata gawio kutoka kampuni Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) lenye umiliki wa UDART, hivyo kushauri Bodi ya wakurugenzi kufuatilia kwa karibu shughuli za UDA.

**HATUA WAZIRI MKUU**

Kuwapo kwa matatizo ya kiufundi na kiutendaji ndani ya kampuni hiyo, kulisababisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, mwaka 2022 kumtumbua aliyekuwa Mkurugenzi wa Fedha na Maendeleo ya Biashara, Suzana Chaula, huku akiweka wazi kuwa tatizo lililoko si uwezo bali usimamzi mbovu.

Majaliwa alifikia uamuzi huo wakati wa ziara aliyoifanya katika kampuni hiyo na kwenye vituo na kubaini utendaji kazi na ufuatiliaji mbovu katika ofisi hizo uliosababisha uwapo wa mabasi mabovu, mifumo ya kielektroniki na mrundikano wa tiketi katika vituo.



Dereva wa pikipiki maarufu bodaboda, akiwa amepakia mizigo na abiria juu, katika barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Baruti, Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Maoni wadau pangua pangua ya Rais

Na Beatrice Shayo

WADAU mbalimbali wametoa maoni kuhusu mabadiliko mapya ya wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri huku baadhi wakisema yanaonyesha umakini wa Rais Samia Suluhu Hassan katika ufuatiliaji wa utendaji wa wateule wake.

Katika mabadiliko hayo yaliyotangazwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, Rais Samia amewateua Luteni Kanali Patrick Sawala kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Paul Chacha (Tabora) na Daniel Chongolo ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mkuu mpya wa Mkoa wa Songwe.

Kabla ya uteuzi huo, Kanali Sawala alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba wakati Chacha alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Misungwi.

Aidha, kutokana na uteuzi huo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Kaban Thomas, na Dk. Frasic Michael wa Songwe uteuzi wao umetenguliwa. Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART).

**MAONI YA WADAU**

Mchambuzi wa masuala ya uchumi, Prof. Haji Semboja, alisema kitendo cha Rais Samia kufanya uteuzi mara kwa mara, kinaleta tafsiri ya kwamba anafuatilia na ana mfumo mzuri wa ufuatiliaji, kudhibiti na kufanya tathmini.

Alisema kuna wakati Rais anapanga timu yake kama timu ya mpira na huo ni kama mchezo wa kisiasa unaoashiria nia ya kubadilisha mfumo wa utendaji wa kazi.

"Unaweza ukaashiria kusema kuna matayarisho fulani ambayo yapo au kuweka timu ambayo itaweza kutimiza malengo ya kisiasa ambayo yamewekwa katika uchaguzi wa CCM. Ninakumbuka uchaguzi upo karibuni hayo ni mabadiliko ya kisiasa haina maana nyingine zaidi ya hayo," alisema.

Prof. Semboja alisema wakuu wa wilaya ni marais wa wilaya na wakuu wa mikoa ni marais wa mikoa, hivyo Rais lazima awe na marais wake wa wilaya na mikoa ambao watatengeneza timu nzuri katika ushindi na kutekeleza mipango ambayo imewekwa katika chama.

"Si unaona katika mpira dakika za mwisho huwa wanabadilishana, waliotoka wameshamaliza mchezo wao na wamewaachia wengine kumalizia game (mchezo)," alisema.

Kuhusu uteuzi wa Chongolo kuwa mkuu wa mkoa, alisema bado alikuwa katika mfumo, hajatoka nje na alikuwa katika tawala za mikoa, hivyo ni mtu ambaye anarudi nyumbani kwake.

"Alivyojiondoa kwenye utawala wa kichama aliona kuna masuala mengine mazuri anaweza kuyafanya akiwa serikalini. Amempeleka serikalini atafanya vizuri pia katika hiyo nafasi," alisema.

Mwanaharakati wa masuala ya kisiasa na kijamii, Bubelwa Kaiza, alisema tangu Rais Samia aingia madarakani kazi yake kubwa ni kuteua kila wakati.

"Ninachokiona (huu) ni mwendelezo wa teuzi, ukichora chati, ukiangalia utendaji wake wa kazi ukiweka majukumu mbalimbali. Jukumu la uteuzi limekuwa juu zaidi kuliko majukumu mengine ukiangalia kuanzia mwaka 2021 hadi sasa kinachoonekana ni kuteua kila baada ya muda fulani,"alisema.

Alisema kuteua, kutengua tafsiri yake anaowateua ni kwamba hakubaliani na kile wanachokifanya au hawatekelezi kama alivyotarajia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) inatakiwa kuwa na menejimenti nzuri na watu wenye utaalamu wa kusimamia biashara ya usafirishaji.

**MA- RC, MA- RAS WAHAMISHWA**

Taarifa hiyo ilisema wakuu wa mikoa wanne wamehamishwa vituo vya kazi. Walioguswa na uhamisho huo na vituo vyao kwenye mabano ni Kanali Ahmed Abbas (Mtwara kwenda Ruvuma), Halima Dendego (Iringa kwenda Singida), Peter Serukamba (Singida kwenda Iringa) Dk. Batilda Buriani (Tabora kwenda Tanga).

Makatibu Tawala wa mikoa waliohamishwa ni Msalika Makungu (Mara kwenda Rukwa), Gerald Kusaya (Rukwa kwenda Mara), Albert Msovela (Kigoma kwenda Katavi), Hassan Rugwa (Katavi kwenda Kigoma), Rehema Madenge (Dar es Salaam kwenda Ruvuma), Stephen Ndaki (Ruvuma kwenda Kagera), na Toba Nguvila Kagera kwenda Dar es Salaam.

MA-DC WAPYA

Katika mabadiliko hayo, pia Rais amewateua wakuu wa wilaya watano. Wakuu hao na vituo vyao ni Abdallah Nyundo (Kilwa), Festo Kiswaga (Monduli), Kanali Alfred Mtambi (Mkinga), Almishi Hazali (Hanang') na Joachim Nyingo (Kilolo)

Mbali na walioteuliwa, pia wamo waliohamishwa vituo ambao ni Deusdedit Katwale (Chato kwenda Tabora), Janeth Mayanja (Hanang' kwenda Chamwino), Julius Mtatiro (Tunduru kwenda Shinyanga), Johari Samizi (Shinyanga kwenda Misungwi), Hassan Bomboko (Ukerewe kwenda Ubungo), Christopher Ngubiagai (Kilwa kwenda Ukerewe), Veronica Kessy (Iringa kwenda Mbulu), Heri James (Mbulu kwenda Iringa) na Paskasi Muragiri (Singida kwenda Bukombe).

Wengine ni Said Nkumba (Bukombe kwenda Chato), Simon Chacha (Sikonge kwenda Tunduru), Hashim Komba (Ubungo kwenda Geita), Cornel Magembe (Geita kwenda Sikonge), Peres Magiri (Kilolo kwenda Nyasa), Kasare Makori (Moshi kwenda Mbinga), Aziza Mangosongo (Mbinga kwenda Mafia), Zephania Sumaye (Mafia kwenda Moshi) na Luteni Kanali Michael Mtenjele (Tarime kwenda Tandahima).

Wamo pia Kanali Maulid Surumbu (Mkinga kwenda Tarime), Zainab Issa (Pangani kwenda Muheza), Faidha Salim (itilima kwenda Busega), Anna Gidarya (Busega kwenda Itilima) Gift Msuya (Chamwino kwenda Bahi), Godwin Gondwe (Bahi kwenda Singida) na Joshua Nassari (Monduli kwenda Magu).

# Wapendekeza viti maalum ubunge, udiwani vifutwe

**Na Enock Charles**

WADAU wa maendeleo ya wanawake wamependekeza nafasi za ubunge na udiwani wa viti maalum vifutwe na kushauri kuwapo nafasi mbadala zitakazogombewa.

Wamesema chanzo cha udhalilishaji kwa wanawake ni viti maalum ambavyo havina hadhi sawa na vile vinavyopatikana kwa kupigiwa kura na wananchi katika majimbo.

Akizungumza katika mdahalo ulioandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) jijini Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Ananilea Nkya, alisema pamoja na suala la udhalilishaji viti maalum havileti uwajibikaji wa moja kwa moja kwa wananchi.

Alisema ni hasara na kupoteza fedha za walipakodi kugharamia viti hivyo.

"Hivi viti maalum vinanikera kabisa na tukiendelea kuving'ang'ania kwamba tunavihitaji sana maana yake tunatangaza kwamba, sisi wanawake hatupo tayari kwenda kufanya uwakilishi ulio sahihi na ambao ni wa uwajibikaji kwa wananchi.

"Sasa hivi bungeni tuna viti maalum 113, wale watu ukifanya hesabu ya haraka haraka kwa miaka mitano ni karibia Sh. bilioni 200.

"Hizi ni fedha nyingi za kodi ya wananchi zinapotea. Mwaka jana serikali ilisema haina Sh. bilioni 35 kulipia bima ya afya watoto wote katika taifa hili, lakini hizo Sh. bilioni 200 zinaweza zikalipia watoto wote bima na zikabaki," alisema Nkya.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Anna Henga, alisema wazo la kuletwa kwa viti maalum lilikuwa ni kuongeza kiwango cha uwakilishi wa wanawake bungeni na kuwajengea uwezo wa baadaye kugombea katika majimbo.

Alisema kwa zaidi ya miaka 50 bado wanawake wameendelea kuwa tegemezi wa viti hivyo jambo ambalo linawalemaza badala ya kuwasaidia.

"Suala la viti maalum lilipokuwa linaanza lilikuwa ni suala la muda kwa kipindi kile kulikuwa na wanawake wachache wamekwenda shule na mifumo iliyokuwapo wakati ule kulikuwa hakuna fursa kwa wanawake," alisema.

Mkurugenzi Henga alisema kwa hiyo wanaharakati wa kipindi kile walipendekeza kuwe na viti maalum kwa muda fulani halafu baadaye wakagombee.

"Changamoto ni kwamba, mtu anakaa miaka 30 kwenye viti maalum, hapo viti maalum vinakuwa havijasaidia. Ndiyo maana wakati wa mchakato wa katiba ilipendekezwa pawapo vipindi viwili vya viti maalum baadaye watu waende kwenye majimbo kwa sababu anakuwa alishapata rasilimali, alishapata mtandao na ujasiri wa kugombea," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum , Ester Matiko, akizungumza na Nipashe, alitaka pawapo kwa nafasi mbadala iwapo viti hivyo vitafutwa kwa kile alichoeleza kuwa, bado kuna uwakilishi usioridhisha wa wanawake katika vyombo vya uamuzi ikiwamo bungeni na kwenye taasisi za serikali na binafsi.

"Mimi ukiniuliza nitakupa mifano ya nchi zingine za Afrika Mashariki Nchi kama Uganda, kuna uwakilishi wa wanawake kupitia wilaya ambao wanapigiwa kura na wilaya nzima kwa hiyo CCM kitaleta mgombea na CHADEMA italeta mgombea wake na vyama vingine kisha wanapigiwa kura na wananchi wote katika wilaya wanawake kwa wanaume" alisema Matiko.



Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya Chama cha ACT Wazalendo, Joram Bashange, akizungumza baada ya kuteuliwa na Kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya chama hicho, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia abeba ajenda nishati safi kupikia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi kuendelea kubeba ajenda ya nishati safi ya kupikia kadri awezavyo, huku akifanya uamuzi mkubwa ukiwamo kuanzisha mfuko wa nishati safi ya kupikia.

Mfuko huo umeanzishwa kwa lengo la kuweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei ya gesi.

Uamuzi mwingine ni kuunda kamati ya kitaifa itakayosimamia utekelezaji wa ajenda na kuchagiza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi za serikali zinazohudumia watu zaidi ya 100 kwa siku.

Akizungumza kwa njia ya simu jana katika kongamano la wanawake la kugawa mitaji na vitendea kazi vya nishati safi ya kupikia la mwaka 2024 lililofanyika jijini hapa, Rais Samia alisema ameona ubunifu wa watanzania katika kuelekea nishati safi ya kupikia.

"Nimeona ubunifu wa watanzania kwenye kuelekea nishati safi ya kupikia, nizungumze na wanawake, jana (juzi) tumemaliza siku yetu. Mimi kiongozi wenu ninabeba ajenda ya nishati safi ya kupikia ndani ya bara la Afrika.

"Mimi ndio championi wake, nimefurahi Wizara za Nishati na Mazingira kuitisha kikao hiki leo (jana) cha nishati safi ya kupikia ambayo wanawake ndio walengwa wakubwa.

"Ahadi yangu, nitaibeba ajenda hii kwa kusaidiana na nyie, kama mnavyojua mwezi Mei tunakwenda kutafuta fedha za kukuza suala la nishati safi ya kupikia Afrika, sasa katika kuibeba hiyo Afrika ahadi yangu nitaibeba nchi yetu kadri ninavyoweza ili kusaidia kuhifadhi misitu na kulinda mazingira," aliahidi Rais Samia.

Akifungua kongamano hilo, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema takribani asilimia 90 ya kaya nchini zinatumia kuni na mkaa kama vyanzo vikuu vya nishati.

Alisema asilimia 65 ya nishati inayotumika majumbani ni kuni, asilimia 26.2 ni mkaa na asilimia 8.8 ni mjumuisho wa gesi, umeme na vyanzo vingine.

Kutokana na matumizi hayo, Dk. Mpango alisema takribani hekta 469,420 za misitu hupotea kila mwaka kutokana na shughuli za kibinadamu ikiwamo ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

"Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) inakadiria thamani ya muda unaotumiwa na wanawake katika kutafuta kuni kuwa na thamani ya takriban Dola za Marekani bilioni 800 kwa mwaka," alisema.

Pia alisema dola trilioni 1.4 kama gharama za matibabu kwa matatizo yatokanayo na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

"Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia nane tu ya watanzania ndio wanatumia nishati safi ya kupikia. Kutokana na hali hiyo, Rais Samia alitoa maelekezo kuhakikisha kuwa, ndani ya miaka 10, asilimia 80 ya watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia,"alisema.

Hata hivyo, Dk. Mpango aliomba wadau kusaidia kampeni ya kuondoa nishati chafu kupitia mikopo midogomidogo, vikoba au vikundi vya kina mama kwa utaratibu wa kukusanya fedha ili kuhakikisha mama anapata vyombo vya ndani.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alitoa rai kwa wanawake wote nchini kuhakikisha ajenda hiyo inakuwa yao kwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili serikali ifanikiwe kuwatua kuni kichwani.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji(EWURA), James Andilile, alisema mamlaka hiyo ina jukumu la kuhakikisha wanamtua mwanamke kuni na mkaa kichwani kwa kutoa leseni kwa wakati kwa wawekezaji kuwekeza katika nishati safi ya kupikia.

Alisema taifa bado linatumia nishati isiyosafi kwa kupikia, hivyo EWURA inatekeleza mikataba ya kukabiliana na kero zinazojitokeza ikiwamo uharibifu wa mazingira na madhara ya afya yanayosababishwa na moshi wakati wa matumizi ya kuni na mkaa.

"EWURA tutahakikisha tunahamasisha uwekezaji katika nishati safi kwa kutoa leseni kwa wawekezaji kwa wakati ili wawekeze katika eneo hilo, pia tunaangalia upatikanaji wake katika maeneo mengi kwa kuangalia mwenendo wa bei za bidhaa hiyo," alisema Andulile.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO
AT MOROGORO

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.2254 OF 2024

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE: KISSA WILSON KULWA

AND

IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY
1. PHOEBE MARTIN KYOMO
2.............................................

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 11 day of 3 /2024.
Dated at Morogoro this 16 day of 02/ 2024.

Resident Magistrate



KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA
LILILOKO DODOMA

MAOMBI NA. 244 YA MWAKA 2023

YAHAYA HASSAN BOLINGO ........................................... MDAI

VERSUS

MWANAIDI HAMISI IDDI........................................... MDAIWA 1

EMMANUEL AMON SIMON....................................... MDAIWA 2

KWA:
MWANAIDI HAMISI IDDI
EMMANUEL AMON SIMON
POPOTE ULIPO

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Dodoma wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 11.03.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa ufike kwa ajili ya kutajwa.
ANGALIZO: Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe **07 ya mwezi wa FEBRUARI, 2024.**

# Simulizi mwanachuo aliyeolewa na nyapala

## - Walikutana gerezani akisubiri kunyongwa hadi kufa

Na Vitus Audax

HAKUNA aijuaye kesho yake. Ndivyo inavyotokea katika maisha ya wengi na wakati mwingine mtu anaweza kukutwa na janga zito hata ndugu zake wakakata tamaa kulikwepa ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu.

Ndivyo ilivyokuwa kwa mwanadada Rose Malle, mkazi wa Moshi mkoani Kilimanjaro ambaye alihukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kukutwa na hatia ya kumuua dereva wa pikipiki maarufu kama bodaboda.

Kutokana na kukutwa na hatia hiyo, inawezekana watu wengi waliamini kwamba adhabu hiyo itatekelezwa lakini ikawa tofauti baada ya kukata rufani kwa msaada wa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kabla ya kukata rufani, alikuwa amekaa gerezani miaka sita kusubiri kutekelezwa kwa hukumu hiyo.

Malle anasema ilikuwa mwaka 2012 alipomchukua dereva wa bodaboda aliyekuwa akimtumia kila siku kwa ajili ya kumpeleka chuoni na dereva huyo wakati anaondoka, alichukuliwa na watu wengine waliomjeruhi kisha kumnyang'anya pikipiki.

Siku iliyofuata, anasema alifuatwa na askari polisi chuoni na kupelekwa kituo cha polisi akituhumiwa kujeruhi na kupora pikikipiki kabla hajafariki dunia.

"Nilishtakiwa kwa kesi hiyo nikapelekwa mahakamani lakini baada ya wiki moja nikarudishwa tena polisi nikabadilishiwa kesi na kuwa kesi ya mauaji baada ya majeruhi kufariki dunia. Hapo kesi ikaanza upya nikawa nahudhuria mahakamani mpaka upelelezi ulipokamilika baada ya miaka miwili na nusu. Kesi ilianza kusikilizwa na baadaye kuhukumiwa kunyongwa baada ya kukaa mahabusu kwa miaka minne kesi ikisikilizwa," anasimulia.

Katika shauri hilo, anasema kabla ya mwendesha pikipiki huyo kufariki dunia, alihojiwa na kutamka kuwa alivamiwa na wanaume wawili lakini kutokana na kuwa binti huyo ndiye aliyemchukua katika kituo chake na kuwa bodaboda wake kila siku, Malle alikuwa mshukiwa wa kwanza hadi kufikia kuhukumiwa.

Anasema alitumikia kifungo hicho kwa muda wa miaka miwili, hivyo kukamilisha miaka sita akiwa gerezani akisubiri siku yake ya kunyongwa na kukatisha ndoto zake za kielimu.

"Siku nahukumiwa, mama yangu alidondoka na kupata mshtuko kisha maradhi ya moyo. Vilevile, nikiwa gerezani baba yangu mzazi alifariki dunia. Sikupata hata nafasi ya kushiriki maziko yake hali iliyozidi kuniumiza zaidi," anasimulia Malle.




TEPF Rose Malle (wa kwanza kushoto) na mumewe (kulia) wakiwa na Ally Athumani ambaye alikuwa mmoja wa wafungwa waliyekutana naye gerezani. **PICHA:VITUS AUDAX**

### MAMBO YALIVYOGEUKA

Historia ya mwanadada huyo ilibadilika baada ya Waziri Mkuu Majaliwa kutembelea gerezani mwaka 2016 kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za wafungwa. Hapo ndipo alipopokewa na kilio cha Malle cha kufungwa bila kosa huku rufani yake ikicheleweshwa.

"Nilihamishwa kutoka Gereza kuu la Karanga na kuhamishiwa Gereza la Isanga mkoani Dodoma. Huko nilikaa kwa mwaka mmoja na nusu na wakati huo nilikuwa bado sijaandika sababu za rufani yangu kutokana na kukosa mwenendo mzima wa kesi yangu," anabainisha.

"Mara ya kwanza alikuja aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mwigulu Nchemba. Nililalamika juu ya kufungwa bila hatia na kucheleweshwa kwa rufani yangu na kipindi hicho gerezani nilikuwa mdogo kuliko wote, hivyo akaagiza jambo hilo lishughulikiwe lakini hakuna kilichofanyika," anasimulia.

Baada ya hapo, anasema maisha yaliendelea gerezani lakini baada ya muda, Waziri Mkuu Majaliwa alifanya ziara gerezani hapo, hivyo kutoa kilio chake kwake kisha (Waziri Mkuu) akatoa siku tatu jambo hilo lishughulikiwe haraka.

"Hapo Waziri Mkuu ndiye alikuja kuwa mkombozi wangu kwani ndani ya wiki, nililetewa mwenendo mzima wa kesi yangu na kuandika sababu za rufani kwa mwanasheria wa magereza zikaenda Arusha. Baada ya wiki moja, nikaletewa tarehe ya kwenda kusikiliza rufani yangu," anasema.

Pia anasema baada ya hapo, alihamishiwa gereza la Arusha na kupata nafasi ya kwenda kusikiliza rufani yake. Siku ya kwanza na ya pili alirudishwa kwa ajili ya kusikiliza hukumu na Wakili wa Jamuhuri alisema hana pingamizi na sababu na mrufani (Malle), hivyo akashinda rufani yake na hatimaye kuachiwa huru.

"Kutokana na madhila niliyopata gerezani, kuambiwa niko huru ilitosha kwangu. Sikuwa na haja hata ya kuanza kushitaki wala kutaka fidia," anasisitiza.

Pia anasema licha kumshukuru Waziri Mkuu kupitia vyombo vya habari kuhimiza jambo lake kushughulikiwa haraka na hatimaye kunusurika adhabu ya kunyongwa hadi kufa, ana shauku ya kukutana naye uso kwa uso ili amshukuru kwa kuwa bila yeye ama angalikuwa bado gerezani au ameshanyongwa.

"Nimeomba nafasi ya kukutana naye nimshukuru kwani bila yeye ningekuwa bado nasubiria siku yangu ya kunyongwa au bado naendelea tu kusota gerezani bila matumaini," anasema.

### ALIVYOPATA MUME GEREZANI

Malle anasema alikutana kwa mara ya kwanza na Mohamed Ulotu akiwa bado mahabusu gerezani Moshi ambaye kwa wakati huo alikuwa akitumikia kifungo cha miaka 30 jela na wakati huo akiwa kiongozi wa wafungwa (nyapara).

Mwanzo wa yote hayo ni wakati alipoomba ruhusa kwa askari wazungumze wakati Ulotu akipeleka wafungwa kupata matibabu katika Zahanati iliyokuwa karibu na gereza la wanawake, hivyo wakabadilishana mawazo na kupeana moyo.

"Mimi niliolewa 2019 kwa kufunga ndoa na ni mama wa watoto wawili kwa sasa," anasema.

Naye Ulotu anasema kwa kipindi hicho ilikuwa vigumu kuwa na uhusiano wakiwa gerezani lakini walizidi kujuliana hali kila walipopata nafasi ya kukutana kwa kuwa si ruhusa kuonekana mfungwa wa kiume na wa kike wakiwa pamoja.

Anasema baada ya kumaliza kifungo chake, aliendelea kumfuatilia Malle akiwa gerezani hadi siku ya rufani yake alikuwapo na kumpa moyo kuwa atashinda. Baada ya kushinda rufani hiyo, safari ya uchumba wao ilianza rasmi kutokana na wote kuwa na nafasi ya kuonana na kuzungumza bila kipingamizi hadi walipofunga ndoa mwaka 2019.

Wawili hao mpaka sasa wamefanikiwa kupata watoto wawili katika ndoa yao na kuendelea na maisha wakijihusisha na harakati za kuwasaidia wafungwa waliomaliza vifungo vyao, wasirejee kwenye uhalifu kisha kurejeshwa gerezani.

### KUSAIDIA WAFUNGWA

Male anasema kutokana na wito huo, waliamua kuanzisha taasisi inayojulikana kama Tanzania Ex-Prisoners Foundation. Lengo kuu la taasisi hiyo ni kuwasaidia wafungwa waliomaliza vifungo ili kuanza maisha ya uraiani kwa kutumia ujuzi walioupata gerezani na kuwaepusha kurudia makosa hatimaye kurudishwa gerezani.

"Idadi kubwa ya mahabusu na wafungwa wanajirudia, hivyo hali hii imetufanya tuanzishe taasisi hii ili kuwasaidia wafungwa kuwa na maisha mapya wanapokuwa uraiani. Tunawawezesha katika mbinu za ufundi na mambo mengine, hivyo tunaomba serikali kupitia wizara husika watusaidie kuinua taasisi yetu kwa hali yoyote ile," anaomba.

Taasisi hiyo inaongozwa na Malle akiwa mkurugenzi na mumewe akiwa katibu.



Rose na mumewe

## HABARI KITAIFA

# Mbeba mkaa afariki purukushani polisi, TFS

**Na Julieth Mkireri,**
BAGAMOYO

MASHAMBULIZI baina ya wabeba mkaa maarufu busta, askari polisi na maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) yaliyotokea Kwala, mkoani Pwani, yamedaiwa kusababisha kifo cha mbeba mkaa na askari kujeruhiwa. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alisema jana kuwa, katika mapambano hayo askari polisi walilazimika kutumia mabomu na risasi, baada ya wabeba mkaa kukaidi kujisalimisha na kuwashambulia askari na maofisa wa misitu kwa mapanga.

Alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana wakati askari polisi kwa kushirikiana na maofisa wa misitu wakiwa doria ya kuzuia uvunaji haramu wa mazao ya misitu.

Kamanda Lutumo alisema katika doria hiyo watuhumiwa saba walikamatwa na magunia 70 ya mkaa pamoja na pikipiki 26.

Alisema awali waliokuwa katika operesheni hiyo walikutana na kundi la watu wakiwa na pikipiki zilizobeba mkaa na walipotakiwa kujisalimisha walikaidi na kuanza kuwashambulia askari polisi na maofisa wa misitu kwa mapanga.

"Kutokana na hali hiyo polisi walijibu (mapigo) kwa kufyatua mabomu ya kishindo na risasi za moto hewani, lakini watu hao wakiendelea kukaidi na kuendelea kukabiliana na askari wakitumia mapanga na visu.

"Katika mapambano hayo askari namba G.7247 koplo Ramadhani (37) alijeruhiwa kwa kukatwa na panga mikononi na kichwani ambapo alikimbizwa Hospitali kwa matibabu.

Kamanda huyo alisema kutokana na tukio hilo, Frank Boniface (33), alikutwa amefariki dunia eneo la tukio na uchunguzi wa kifo hicho unaendelea.

Wakizungumzia tukio hilo, madereva wa bodaboda walisema tukio hilo lilitokea majira ya saa sita usiku wakati wakiwa kwenye safari wakitoka msituni ndipo walipokutana na gari ambalo lilikuwa na askari wa misitu ambao walifyatua risasi.

Abison Songa, mmoja wa madereva pikipiki ambao waliamua kusitisha safari yao katika Kijiji cha Kwala baada ya tukio hilo, alisema wamekuwa wakikumbana na matukio hayo mara kwa mara na kudai kuwa, baadhi yao hupoteza maisha.

Songa aliiomba serikali kuridhia kuwapatia vibali vya kusafirisha mkaa kama vinavyotolewa kwenye magari na toyo ili kuepusha sintofahamu za mara kwa mara. Sabas Enock, alishauri suala hilo litafutiwe ufumbuzi kwa kuwa, limekuwa chanzo cha ongezeko la majeruhi madereva wa bodaboda na vifo.

Katibu wa umoja wa madereva bodaboda wabeba mkaa hao, Ramadhani Msemakweli, alisema tukio hilo ni la tano kutokea na sababu kubwa ni kutokana na kukosa vibali vya biashara hiyo.

Ramadhani alisema kwa sasa idadi yao inafikia 200 na hawana kazi ya kufanya zaidi ya biashara hiyo ya mkaa, huku wakala huo ukisisitiza kuachana na biashara hiyo badala yake watumie magari badala ya bodaboda.

"Sisi tuko tayari kulipa ushuru unaotakiwa wa halmashauri na serikali kuu na tuko tayari kupunguza ukubwa wa magunia kama itahitajika kufanya hivyo. Cha kushangaza ni kwamba, tatizo hili ni kwa Mkoa wa Pwani pekee, wakati ipo mikoa mingine ambayo kuna madereva wanaosafirisha mkaa kama sisi," alisema.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kwala. Salumu Bai. alisema usiku wa kuamkia jana, alisikia milio ya risasi na asubuhi alipokwenda eneo la tukio alikuta mwili wa kijana mmoja wa bodaboda anayedaiwa kupoteza maisha kwa madai ya kupigwa risasi na askari wa misitu.

Januari, mwaka huu, mvutano baina ya askari sita wa TFS na vijana wanne wabeba mkaa ulioibuka eneo la Tegeta Machinjioni, Dar es Salaam, ulisababisha asiyehusika kujeruhiwa kwa risasi kwa madai ya askari hao kufyatua risasi na kumjeruhi muuza nyama.




Kijana akiosha kioo cha gari lililokuwa limesimama katika mataa ya makutano ya barabara za Sam Nujoma na Bagamoyo, eneo la Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar as Salaam jana, ili kujipatia ujira wa siku. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Pinda ataka hatua dhidi ubaguzi kijinsia

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKE wa Waziri Mkuu Mstaafu, Tunu Pinda, ameishauri serikali na taasisi zake, wadau wa maendeleo na wananchi kuchukua hatua dhidi ya masuala ya ubaguzi wa kijinsia na uonevu unaofanywa kwa wanawake.

Akizungumza juzi katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani Ikungi mkoani humo alisema Tanzania inaunga mkono jitihada za kimataifa za kukuza usawa wa kijinsia.

Maadhimisho hayo yamebebwa na kaulimbiu isemayo "Wekeza kwa mwanamke kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii,".

Tunu alisema pia Tanzania imejielekeza katika utekelezaji wa mikakati ya kufikia kizazi chenye usawa.

Alisema katika kutekeleza hilo, Desemba 16, 2021, serikali ilizindua Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya utekelezaji wa ahadi za nchi kuhusu kizazi chenye usawa.

Alisema kuanzishwa kwake ni jitihada za serikali katika kutoa msukumo wa utekelezaji wa masuala ya haki na usawa kwa wanawake na wanaume.

Tunu alisema lengo kuu la kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ni kutoa fursa kwa jamii kupima utekelezaji wa maazimio, matamko, mikataba na itifaki mbalimbali za kimataifa, kikanda na kitaifa zinazohusu masuala ya maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wanawake.

Alisema kufanya hivyo ni kuhakikisha kuwa haki za wanawake kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kisiasa zinapatikana na zinalindwa.

Pia alisema kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kutambua na kuthamini uwezo na mchango mkubwa wa wanawake katika kuleta maendeleo.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Mendeleo Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, inatambua umuhimu wa wanawake wote na wajasiriamali kuwa ni miongoni mwa watu muhimu katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na pato la taifa.

Alisema katika kutambua hilo imewekeza kwa wanawake kwa kuimarisha mfumo wa utoaji mikopo kwa wanawake, kufanya marekebisho ya sheria ya fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (2018) ambayo kifungu cha 37A kinazielekeza mamlaka husika kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu.

"Ninatoa rai yangu kwa wanawake wa Mkoa Singida kujitokeza na kuzifanyia kazi fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ili kuweza kufikia malengo ya usawa wa kijinsia kwa maendeleo endelevu," alisema

Kuhusu vitendo vya ukatili, Tunu alisema serikali inatambua jukumu hilo si la mtu mmoja au kikundi kimoja cha watu, bali ni la kila mmoja kwa nafasi yake.

Tunu alisema serikali imeandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) II kuanzia 2022/2023 hadi 2027/2028.

# CCM: tunatambua mchango wanawake

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kinatambua mchango uliotolewa na wanawake nchini tangu wakati wa harakati za uhuru hadi sasa kuna maendeleo makubwa na mabadiliko katika sayansi na teknolojia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, CCM chini ya Mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan, kinawatakia wanawake wote wa Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla maadhimisho mema ya siku ya wanawake duniani.

"Kupitia kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inayosema siku ya wanawake duniani, wekeza kwa wanawake kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii.

"Chama kinapenda kutoa wito kwa jamii nzima ya Watanzania kuendelea kuhamasisha na kuhimiza umuhimu wa kufanya uwekezaji wa kijamii, kisiasa na kiuchumi bila kubagua jinsia ya watu wanaounda jamii ambao ni mwanamke na mwanaume,"alisema Makonda.

Alisema CCM imepewa dhamana ya kutoa uongozi wa nchi, inatambua mchango uliotolewa na wanawake nchini toka harakati za uhuru hadi sasa.

"Tumefikia maendeleo makubwa nchini hasa katika nyakati hiki cha maendeleo na mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia pale taifa na jamii kwa ujumla vinaposhindana mapambano ya ubaguzi wa kijinsia, halikadhalika yanapatikana kwa haraka wanawake wanapokuwa katika uwekezaji unaofanywa," alisema.

Makonda alisema CCM kupitia mwenyekiti wake, kinatoa wito kwa watanzania wakiwamo wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali katika chaguzi zijazo bila ubaguzi wowote.

Alisema wapo pamoja na wanawake wote wa Tanzania, Afrika na duniani kote katika maadhimisho hayo wakiwatakia maadhimisho yenye amani, upendo na utulivu katika kutafakari maendeleo ya mataifa na ustawi wa jamii wanayoi-

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko ya Rais yawe funzo kwa wateule wapya, walio kazini

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, jana alifanya mabadiliko ya wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri. Katika mabadiliko hayo, kuna sura mpya zimeingia huku baadhi ya wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi katika baadhi ya maeneo wamehamishwa vituo vya kazi huku wengine wachache uteuzi wao ukitenguliwa.

Hii si mara ya kwanza kwa Rais Samia, ambaye hivi karibuni anatarajia kutimiza miaka mitatu akiwa katika nafasi hiyo kufanya mabadiliko ya namna hiyo. Amefanya mara kadhaa huku mambo kama hayo yakitokea kwa watu wapya kuteuliwa, wengine kuhamishwa kwenye nafasi zao na kupangiwa majukumu mengine.

Kila anapofanya mabadiliko kwa kuteua, kuhamisha na kutengua pamoja na kuwapandisha wengine, Rais amekuwa akitoa sababu zikiwamo miongoni mwa wateule wake kutokwenda na kasi anayoitaka, kushindwa kutimiza wajibu wao ipasavyo na masuala ya nidhamu. Kwa maneno mengine kwenda kinyume cha maadili na miiko ya uongozi kama ambavyo wamekuwa wakiapa.

Sababu nyingine ambayo amekuwa akiitoa mara kwa mara Rais Samia ni kuimarisha utendaji kazi katika ngazi mbalimbali serikalini na kwamba anapoona mahali fulani panapwaya, hana budi kufanya mabadiliko.

Katika mabadiliko ya jana kwa mfano, waliokuwa wakuu wa wilaya wawili, wamepandishwa kuwa wakuu wa mikoa huku wawili waliokuwa katika nafasi hiyo wakiondolewa. Mmoja uteuzi wake umetenguliwa na mwingine kupewa majukumu ya kuiongoza taasisi nyeti ya serikali ambayo imekuwa ikilalamikiwa kuwa na changamoto mbalimbali.

Sambamba na eneo hilo, wako wakurungezi wa halmashauri ambao wameondolewa na hakuna sababu zilizotolewa na pia wamo wapya walioteuliwa kuchukua nafasi hizo. Wengine kutoka kituo kimoja kwenda kingine kwa nafasi za ukuu wa wilaya na wakurugenzi wa mamlaka hizo za serikali za mitaa.

Mabadiliko hayo ambayo yamekuwa yakifanyika mara kwa mara, yanapaswa kuwa funzo kwa wateule mbalimbali wa Rais kwenye maeneo tofauti. Ni wazi kwamba Rais anapofanya mabadiliko ya uteuzi wa watu wa kumsaidia katika nafasi hizo, anakuwa na imani kwamba watamsaidia katika azma yake ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma na maendeleo katika sekta mbalimbali kama vile afya, elimu, miundombinu na maji.

Pia Rais amekuwa akihimiza wateule hao kufanya kazi kwa weledi na kutatua kero za wananchi kwa kutembelea maeneo yao ya utawala ili kuyatafutia majawabu matatizo hayo. Lakini kinyume chake, miongoni mwa wateule hao wamekuwa wakishindwa kufanya hivyo na kukaa ofisini kama miungu watu huku wakitaka kusujudiwa na hata kujinufaisha na nafasi hizo.


Kama wahenga wasemavyo siku zote binadamu anajifunza kutokana na makosa, ni vyema wateule hao wapya na wale waliopandishwa na kubadilishwa vituo vya kazi, wachukue hatua kujifunza na kutimiza mambo ambayo mteuzi wao amekuwa akiwataka wayafanye.

Hivi karibuni, kwa mfano, Katibu wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC) ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, alifanya ziara katika mikoa kadhaa na kubaini madudu ikiwamo wananchi kudhulumiwa haki zao kama vile ardhi huku baadhi ya maofisa waliopewa dhamana wakituhumiwa kushiriki.

Kwa mantiki hiyo, haiwezekani wateule wa Rais wawapo katika sehemu husika ambayo wananchi wanalalamika kunyanyaswa na kuonewa bila kuchukua hatua zozote au wakiwasilishiwa matatizo hayo, wanakuwa sehemu ya kuongeza kero badala ya kutatua. Jambo hilo haliwezekani na pindi linapobainika ni lazima Rais achukue hatua za kuwatumbua kama ambavyo amekuwa akifanya mara kwa mara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Sabato Kasika

# Wanasiasa msipotoshe wananchi, maendeleo hayana chama

**TANGU** kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa zaidi ya miaka 30 iliyopita, kumekuwapo na kauli za rejareja kutoka kwa baadhi ya wanasiasa ambazo huenda hutokana na ulevi wa madaraka ambao husababisha waseme lolote watakavyo, bila kupima madhara yake.

Moja ya kauli hizo ni kuwataka wananchi kutokuchagua wapinzani, kwa maelezo kwamba serikali haitopeleka huduma muhimu kwenye maeneo yatakayokaliwa na viongozi wasiotokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Lakini pia kauli nyingine ambayo imewahi kutolewa na mkuu mmoja wa mkoa ni ya kuwataka madiwani wa upinzani kujiunga CCM ili ashirikiane nao kutekeleza ilani ya chama hicho tawala.

Kwa ujumla ni kwamba kauli za aina hiyo zimewahi kutolewa na makada wengi wa CCM na hata wiki iliyopita, mwenyekiti wa CCM wa mkoa mmoja alikaririwa na vyombo vya habari akionya wananchi.

Mwenyekiti huyo alitoa onyo kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, tishio likiwa ni kwamba wakichagua upinzani, serikali haitopelekea huduma muhimu.

Ninadhani kauli hizo zinaonyesha kuwa wanaozitoa hawajui kwamba nchi iko ndani ya mfumo wa vyama vingi, ambao serikali wanadai haitapeleka maendeleo, iliuridhia tangu mwaka 1992.

Labda niwakumbushe kuwa, Ibara ya 8 ya katiba ya Tanzania inaelekeza kuwa (a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba, (b) lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi (c) serikali itawajibika kwa wananchi.

Kwa maana hiyo, wananchi wenyewe ndio wanaochagua viongozi kuanzia ngazi ya vitongoji hadi taifa, hivyo uamuzi ni wao wachague kiongozi wanayemtaka bila kuelekezwa au kushinikizwa.

Iwapo wataadhibiwa kwa kutopelekewa maendeleo kutokana na uamuzi wa kuchagua upinzani, hata urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi, ili kuwapa fursa ya kuchagua ndani au nje ya CCM, hautakuwa na maana.

Sidhani kama maendeleo yanaletwa kwa kuchagua wagombea wa CCM tu, bali yanaletwa na Watanzania wote kupitia kodi zao na sio kupitia chama kama ambavyo baadhi ya wanasiasa wanataka kuwaaminisha.

Kimsingi uongozi ni nyenzo muhimu ya kufikia maendeleo. Hata Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, enzi za uhai wake aliwahi kusema, ili nchi ipate maendeleo inahitaji vitu vinne ambavyo ni watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Vitu hivi vinne kwa pamoja vikitumika kama inavyotakiwa, vinaweza kuwa nyenzo madhubuti ambayo itasaidia kuharakisha maendeleo na ustawi wa maisha ya Watanzania bila kujali itikadi za vyama vyao.

Kutokana na umuhimu huo, ndio maana Rais Samia Suluhu Hassan amedhihirisha kuwa ni kiongozi anayefanya juhudi za kuhakikisha nchi inapiga hatua za kimaendeleo kwa kuleta umoja na mshikamano nchini.

Yeye anazingatia kuwa ujenzi wa taifa unahitaji mchango wa kila mwananchi bila kujali tofauti za kisiasa, dini, jinsi, ukanda, amekuwa akisisitiza na kuishi maneno yake ya kuhimiza umoja wa kitaifa.

Aidha, Rais amekuja na falsafa katika ujenzi wa nchi aliyoipa jina la 4R za maneno ya Kiingereza za Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko) na Rebuiding (Kujenga upya).

Wakati akiendelea kusimamia falsafa hiyo, wanajitokeza baadhi ya makada ambao wanaweza kuifanya isionekane ina maana iwapo hawataelekezwa kuacha 'kutisha' wananchi.

Maridhiano (Reconciliation) ni kitu muhimu katika ujenzi wa taifa ili kuwa na sauti moja, Rais Samia anaamini maridhiano na maelewano yanawezekana kwa kukaa pamoja na kujadiliana kwa njia ya mazungumzo na ya amani.

Ni wazi kwamba palipo na maridhiano kuna maelewano, palipo na maelewano kuna amani na kuna kusonga mbele kimaendeleo, kwani maridhiano yanachagiza usuluhishi wa tofauti za kisiasa ili kushirikiana kwa kujenga nchi kwa pamoja bila kubaguana.

Kwa kuheshimu hayo, Rais Samia ameshakaa meza moja na viongozi wa vyama vya upinzani ili kuwa na maridhiano yaliyolenga kutibu majeraha ya kisiasa kama ishara ya kufungua ukurasa mpya.

Ukarasa huo mpya ni wa kujenga umoja wa kitaifa, hivyo itapendeza iwapo makada wa CCM ambao bado wana viashiria vya ubaguzi wa itikadi za vyama wakaunga mkono juhudi za Rais.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Wanawake wajitokeze tuwachague kufikia 50/50, tufute viti maalumu



Pascal Mayalla

**Baadhi ya wanawake baada ya kushika nafasi fulani fulani kwa upendeleo, wakaonyesho uwezo mkubwa kuliko hata wanaume. Japo kazi ni kazi tu, hakuna kazi za kike wala za kiume je, kuna ukweli kuwa kwenye baadhi ya kazi, wanawake wana uwezo nazo kuliko wanaume?**

JUZI, Watanzania tulijumuika na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wa wanawake katika maendeleo ya dunia hii.

Kwa mantiki hiyo, naomba nianze kwa kuwapongeza wanawake wote duniani kwa kuadhimisha siku yao hii. Hongera sana wanawake wote. Bila wanaume, maisha bado yanawezekana lakini bila wanawake, maisha hayawezekani. Kwa hiyo wanawake ndio watu wa muhimu zaidi duniani kuliko hata wanaume, lakini siku zote wamekuwa hawapewi nafasi stahiki kwenye jamii.

Adui mkubwa wa usawa wa kijinsia ni uwapo wa mfumo dume ambao umeanzia kwenye dini kwa kuelezwa hapo mwanzo Mungu aliumba mwanamume tu, kisha akaona si vyema mwanamume aishi peke yake, akamfanyizia msaidizi kutoka kwenye ubavu wake, hivyo jamii nyingi zinaamini mwanamke ameumbwa ili kumsaidia mwanamume.

Jamii nyingi za Kiafrika zimeathiriwa na mfumo dume kwa kumwona mwanamke ni kiumbe dhaifu na kiumbe dhalili. Hata katika malezi na makuzi, mtoto wa kiume analelewa kujitegemea na hata akiumia au akifiwa, anakatazwa kulia kwa sauti kuwa usiwe kama wanawake ndio wanalia, Mwanamume gangamala. Mwanamume alihesabika ndiye ameumbwa kuhangaika na nafasi ya mwanamke ni jikoni!

**MWANZO VITI MAALUMU**

Kutokana na dhana hii ya mwanamke ni dhaifu, hawezi kugombea nafasi na kushindana na mwanamume akashinda, ndipo ukabuniwa utaratibu maalumu uitwao 'affirmative action' ili wanawake wapate nafasi kwenye baadhi ya maeneo. Walihitaji nafasi za upendeleo ndipo viti maalumu vikabuniwa.

Baadhi ya wanawake baada ya kushika nafasi fulani fulani kwa upendeleo, wakaonyesho uwezo mkubwa kuliko hata wanaume. Japo kazi ni kazi tu, hakuna kazi za kike wala za kiume je, kuna ukweli kuwa kwenye baadhi ya kazi, wanawake wana uwezo nazo kuliko wanaume?

Japo kazi ni kazi na wanaume wanajihesabu kuwa wao ndio watenda kazi na wachapa kazi hodari kuliko wanawake, yaani ni watu wa kuchuma na wanawake ni watu wa kupokea, siku hizi kuna wanawake ndio wachumaji na 'vibenten' vinalelewa!

Kuna kazi mfumo dume umezipachika kuwa ni kazi za kike zikiwamo upishi, ubunifu wa mavazi, ususi na kazi za kuremba wanawake, lakini imetokea wapishi wote wa hoteli kubwa ni wanaume! Wabunifu wakubwa wa mavazi ni wanaume hata warembeshaji wakubwa na sasa wasusi ni wanaume!

Huu mfumo dume umesababisha baadhi ya nafasi kupewa majina ya kiume mfano 'bosi' ni jina la kiume. Bosi akiwa ni mwanamke anaitwa 'The Boss Lady' lakini mabosi wa kike wanapenda kuitwa na wafanyakazi, wengi wanaamini bosi awe mwanamume na si mwanamke. Wanaamini kuwa bisi akiwa mwanamke, basi watu watakoma!

Pia nafasi kama ya mwenyekiti kutokana na mfumo dume ilionekana kuwa ni ya mwanamume. Takribani miaka mitatu iliyopita, Tanzania ilipata Rais mwamamke, ukaibuka mjadala kwa kuwa Rais pia ni Amiri Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama na miaka yote iliozoeleka Rais ni Mwanamume, itakuwaje?

Ikaja hoja kwamba Amiri jeshi Mkuu anaitwa hivyo kama ni mwanamume na mwanamke anaitwa Amirati lakini hata Amiri Jeshi Mkuu anapokuwa Mwanamke, hapendi kuitwa Amirati anapendelea kuitwa Amiri jeshi ambalo ni jina la kiume au 'chairman' badala ya 'Chairwoman' au 'chairperson'.

Tukubali tukatae bado tuna baadhi ya watu miongoni mwetu, waliofilisika kifikra na kisiasa ambao bado wana tatizo la kutawaliwa na mfumo dume vichwani mwao na kuamini urais wa nchi ni kazi ya kiume!

Hali hiyo inanifanya nijiulize kuna ukweli wowote kuwa kuna kazi za kiume na za kike na kuna kazi za kike ambazo ni za kike tu? Pia je, kuna kazi za kiume ambazo wanawake hawawezi?

Baada ya Tanzania kupata Rais mwanamke kwa kudra tu ya Mwenyezi Mungu, natoa wito kwa Watanzania kumchagua rasmi Rais mwanamke katika uchaguzi mkuu wa 2025. Je, mnaonaje kama pia tumchagulie na wabunge na madiwani wanawake wa kutosha kufikisha ile idadi ya asawa ya kijinsia wa asilimia 50/50?

Na hiyo aslimia 50/50 ikiishafikiwa na kupatikana, bado kuna haja ya kuendelea na ubunge na udiwani wa viti maalum kwa wanawake? Watakuwa wa nini?. Mnaonaje baada ya kufikiwa kwa idadi ya 50/50 na kukidhi usawa wa kijinsia, tuvifute viti maalumu kwa sababu tayari tutakuwa tumefikia usawa wa kijinsia kwa mujibu wa mkutano wa Beijing?

Kwa sababu wanawake wa kukidhi asilimia 50/50 wapo, wahamasishwe, wajitokeze, na Watanzania tuwachague. Baada ya kufikiwa 50/50, kwa mtazamo wangu viti maalum vifutwe.

**Wasalaam.**
**Paskali**
**0754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Tayari tunaumwa kiuchumi, msituroge kisiasa



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

SI siri kwamba idadi kubwa ya Watanzania tunapitia kipindi kigumu kiuchumi ingawa kisiasa tumetulia licha ya kuwapo baadhi ya watu wanaotaka kuchokonoa makovu.

Kipindi hiki ni kigumu kutokana na madhila tunayopitia, yakiwamo ya umeme, maji na hata sukari ambayo imekuwa wimbo huku wakazi wa Dar es Salaam wakiongezwa adha ya mabasi yaendayo haraka.

Ingawa kuna unafuu kidogo wa umeme, lakini kipindi kifupi kilichopita, tulionja 'joto ya jiwe' na kila mtu mahala pale akilia na TANESCO ambao nao waliamua kuziba masikio na kusonga mbele kivyao.

Kadhia ya maji hivi sasa ni kubwa ni kawaida hivi sasa maji yakitoka ndipo watu wanashangilia kama walivyoshangilia umeme ulipokuwa ukirudi jioni au asubuhi, baada ya kukatika mchana kutwa au usiku kucha mtawalia.

Mabomba mengi hayatoi maji ingawa wahusika awali walisingizia kukatika umeme kama ambavyo wa umeme walivyokuwa wakisingizia ama ukarabati wa mitambo au ukosefu wa maji kwenye mabwawa.

Wanaosimamia maji sasa wanasema miundombinu ya maji imevurugwa na mvua zilizonyesha na kufukua mabomba na kwingine kuyakata, na sasa yanachomelewa na mafundi wachomeleaji vyuma.

Kwenye sukari huko usiseme kabisa, unashuhudia wafanyabiashara wakifanya wapendavyo, licha ya Bodi ya Sukari ikishirikiana na viongozi wa serikali kupambana nao kwa kuwakamata na kuwafikisha Polisi.

Ukitazama sura za wafanyabiashara unaona kabisa hawana wanachoogopa zaidi ya kuhofia maisha yao tu, lakini wako tayari kukabiliana na lolote ili mradi wanauza sukari tofauti na bei elekezi ya serikali.

Ukikaa na kujiuliza inakuwaje nchi hii yenye umri wa mzee mzima wa zaidi ya miaka 60 bado inasuasua kwenye huduma za maji, umeme na hata vitu kama sukari na kuishi kwa kuagiza nje ya nchi, hupati jibu.

Unaweza kujiuliuza kwa nini huko nyuma mambo haya hayakuwapo, hususan kipindi cha karibuni cha utawala wa Dk. John Magufuli mambo kama haya usingeyasikia.

Inawezekana kabisa watu wameaua kumpima ubavu Rais Samia Suluhu Hassan kwamba atawafanya nini, kwa sababu haiwezekani vilio vingi vya Watanzania kuishia hewani na kuendelea kutaabika kwa mambo yaliyo ndani ya uwezo wa serikali.

Kunaweza kusitokee ubishi, kama mtu atatwambia kuwa baadhi ya wateule wa Rais Samia wanajifanyia wanavyojua wao kwa maslahi yao kwani hawaumii hata kidogo kutokana na matatizo yaliyopo.

Wanaishi wanakula, wanavaa, wanasomesha watoto wao wanakotaka wana magari wana kila kitu, wanalala kwa raha na kuamka na furaha, huku masikini wakiteseka na wao wakiendelea na uhakika wa ajira zao.

Wakati mwingine huwa najifikirisha kwamba mathalan nchi ikiendeshwa kama baa, ambako wahudumu hupangiwa malengo ya kufanya na kulipwa kwa walichofanya ingekuwaje?

Kwamba mhudumu anapewa masanduku idadi fulani ya bia au soda na kuambiwa utauza kulingana na chupa ulizouza, hivyo hivyo iwe kwa viongozi wa nchi kwamba unapewa malengo haya usipoyatimiza hulipwi mshahara, ingekuwaje?

Au mathalan bungeni, mbunge anapangiwa utauliza maswali kadhaa au kuchangia hoja kadhaa asipotimiza halipwi mshahara, ingekuwaje? Lakini kwa kuwa mishahara na posho ziko palepale, hata mtu asipotimiza atalipwa, basi bora liende.

Kwa hali hii, hivi nani atapoteza muda na nguvu zake kupiga makelele au kusafiri kwenda kusikilkiza kero za wananchi wakati anajua atalipwa tu hata akilala mchana kutwa, usiku kucha bila kufanya kazi!

Pengine ndiyo sababu Rais kaamua kwamba sasa atakuwa anakutana na wananchi angalau mara moja kwa mwezi kusikiliza kero zao. Utadhani hana wawakilishi alioteua mikoani na wilayani!

Lakini wakati tunakabiliwa na hali ngumu kiuchumi, kuna watu wanaibuka sasa kukumbushia madonda ya zamani kisiasa. Hivi Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa mkoa anapoibuka na kusema waliko wapinzani huduma zisipelekwe, anataka nini?

Hii dhana ilihubiriwa sana na Dk Magufuli watu tukamshangaa kuwa ni kiongozi mbaguzi tu ndiye anayeweza kuyafanya haya, lakini kaibuliwa mwingine wa CCM iliyojisahaulisha aliyoyafanya huko nyuma, na sasa anaibuka na kauli kichefuchefu kama hizi! Tumkatalie kabisa kutugawa Watanzania.

Hana tofauti pia na kiongozi wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM ambaye naye kaibuka usingizini na kuwaambia wanawake wenziwe, kuwa wasichague wanaume kwenye uchaguzi. Huyu anataka nchi hii iongozwe na wanawake tupu! Hawa ni wanasiasa uchwara waliojisahau. Mungu walaani tu hawa!

## Wanafunzi mahitaji maalumu wakumbukwa

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani, wanafunzi wasichana wenye mahitaji maalumu wa Sekondari ya Jangwani Dar es Salaam, wamesherehekea siku hiyo kwa furaha zaidi baada ya kuungwa mkono na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA), katika kuwaboreshea masomo na maisha yao.

Wanawake wa TFRA wakiongozwa na Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa TFRA, Victoria Elangwa, juzi waligusa mioyo ya wasichana 110 kutoka mikoa mbalimbali wanaosoma Jangwani kwa kuwapa mahitaji ya usafi na ya kitaaluma, yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni mbili pamoja na kuwandalia chakula cha mchana.

Akizungumza katika hafla ya kusherehekea na wasichana hao, iliyofanyika shuleni hapo, Elangwa alisema mamlaka hiyo imetumia siku hiyo kuwafikia wanafunzi hao wanaoishi na ulemavu na wengine wa Shule ya Msingi Temeke.

Alisema ni kawaida yao kutoa elimu kwa wanafunzi kuhusu matumizi bora ya mbolea ambao ndiyo wakulima wa kesho.

Aidha, wakiwa Jangwani, aliwapongeza wanafunzi hao kwa kuthibitisha kuwa kuishi na ulemavu si kushindwa maisha.

Aliwasifu kwa juhudi zao kitaaluma kwa kusoma tahasusi za sayansi, uchumi, hesabu,biashara na sanaa na kuwaeleza kuwa wajitahidi kwani ndiyo sehemu ya wataalamu wa taifa la kesho.

Baadhi ya vifaa walivyopokea wanafunzi hao kwa mujibu wa Victoria ni daftari, kalamu, mikebe ya vifaa vya hesabu, karatasi (rim papers), rule na vichongea kwa ajili ya masomo.

Aidha, wamepewa pia vifaa vya usafi binafsi kama sabuni za kuogea, mafuta ya kupaka na karatasi za vyooni. Ili kusafisha maeneo yao wamepewa, mafagio, sabuni za maji na za unga na madekio.

Meneja wa Uhusiano na Mawasiliano wa TFRA, Matilda Kassanga, aliongeza kuwa kama taasisi ya umma inawajibika kujenga mahusiano mazuri na wadau wengine zikiwamo taasisi za serikali na binafsi na hivyo kurudisha fadhili au shukrani kwa jamii.

Alisema:"Ujio wa wanawake wa TFRA shuleni hapa ni kuongeza hamasa zaidi kwa wanafunzi wa kike kuzifikia ndoto zao katika Nyanja mbalimbali ikiwamo uongozi."

Alisema wanatambua kuwa wasichana hao ni wamama wa kesho, lakini pia ni wataalamu wa fani mbalimbali wanaotegemewa na taifa, hivyo wanawake TFRA wanawapa hamasa zaidi kufikia mafanikio katika masomo yao .

"Tunapenda tuwe mifano kwao (role model) kuwahamasisha kufikia mafanikio kitaaluma na pia kuwa raia na wataalamu bora." Alisema Matilda.

Makamu Mkuu wa Sekondari ya Jangwani, Paulina Aweda, akiwashukuru wanawake wa TFRA, alitoa wito taasisi nyingine kuunga mkono wanafunzi wahitaji kwa kuwasaidia chochote walichonacho.

Alisema sekondari hiyo inatoa elimu jumuishi inayohusisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

# Wanaume wakumbukwa usawa kijinsia

**Na Augusta Njoji,**
CHAMWINO

SERIKALI imezindua Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake 2023 ambayo pamoja na mambo mengine imetoa kipaumbele cha ushiriki wa wanaume katika jitihada za kujenga usawa wa kijinsia.

Pia, imetoa kipaumbele kwa wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu, huku jamii ikiaswa kuondokana na dhana iliyojengeka kuwa wanawake hawatakiwi kuwa viongozi.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa sera hiyo kwa niaba ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya wanawake duniani iliyofanyika kimkoa wilayani hapa.

Alisema sera hiyo imeboreshwa ili kuendana na hali ya sasa na ni muhimu katika kukuza usawa wa kijinsia.

"Ni matumaini yangu kuwa sera hii itatuvusha katika kipindi kingine kirefu katika utekelezaji wake ili kuendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo na Malengo ya Dunia kuhusu usawa wa kijinsia, ninatoa rai kwa wadau kuhakikisha wanatoa ushirikiano katika utekelezaji wa sera hii,"alisema.

Kadhalika, alisema serikali kwa kushirikiana na taasisi za fedha imeanzisha madirisha maalum ya kuwezesha wanawake kupata mikopo yenye riba nafuu ili kupunguza umaskini kwa wanawake kwa kuwawezesha kupata mitaji.

"Madirisha hayo ni pamoja na Mwanamke Hodari (Benki ya Azania), Jasiri Bondi (Benki ya NMB), Malkia Bond (CRDB) na Johari (NBC) ambayo yanatoa mikopo kwa riba nafuu.

"Dirisha la wanawake katika Benki ya Biashara Tanzania (TCB) linaunganisha linalotoa mkopo yenye masharti nafuu kwa wanawake katika mikoa yote nchini,"alisema.

Alisema mikopo hiyo imewaewezesha wanawake kupata mitaji na kujishughulisha na biashara.

Aidha, alisema serikali imeendelea kuchukua jitihada mbalimbali za kuhakikisha kuwa, wanawake wanapata fursa na haki sawa katika nyanja zote.

Alibainisha kuwa serikali katika kutatua malalamiko ya wananchi katika maeneo mbalimbali hapa nchini, iliamua kuanzisha kampeni ya msaada wa kisheria ijulikanayo kama Mama Samia Legal Aid Campaign, ikiwa ni jitihada katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za kisheria kwa wananchi wasio na uwezo.

"Kampeni hiyo inaendelea vizuri na kwa namna ilivyopokelewa ni wazi kuwa, kuna uhitaji mkubwa wa msaada wa kisheria hapa nchini.

"Tayari imewafikia wananchi 383,293, wengi wao wakiwa ni wanawake katika mikoa sita ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu na Singida,"alisema.

Alisema kupitia kampeni hiyo, migogoro takribani 511 ilitatuliwa na imewasaidia kubaini maeneo yaliyo na migogoro mingi zaidi kwenye jamii ambayo ni ardhi, matunzo ya watoto, ndoa, mirathi na ukatili wa kijinsia.

Awali, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jinsia, Badru Abdulnuru, alisema sera hiyo imeweka malengo na matamko mahususi ya kisera yatakayowezesha kukabiliana na kero za masuala ya jinsia na uwezeshaji wa wanawake nchini kwa ufanisi mkubwa.

Alitaja masuala yaliyojumuishwa kwenye sera hiyo kuweka matamko mahsusi ya kisera yenye masuala ya kijinsia ambayo hayakuwapo; Kuongeza wigo wa matamko ya kisera yaliyopo ili kujumuishwa katika maeneo mengine ikiwamo jinsia na takwimu na umuhimu wa ushiriki wa wanaume katika jitihada za kufikia usawa wa kijinsia;

Nyingine ni kujumuisha mipango ya maendeleo ya kitaifa, kkujumuisha baadhi ya mikataba na makubaliano pamoja na itifaki za kikanda na kimataifa inayohusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake ikiwamo ajenda ya kufikia uwiano wa 50/50 ifikapo 2030.




Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Rachel Mhavile (kulia), akipokea msaada wa 'microwave' kutoka kwa Meneja Biashara wa Benki ya Diamond Trust (DTB), Georgina Alfred iliyotolewa na benki hiyo, kwa ajili ya matumizi ya wauguzi na madaktari hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam juzi, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MARY KADOKE**

# Polisi, waandishi wakubaliana kuzingatia weledi

**Na Joseph Mwendapole**

JESHI la Polisi Kinondoni limekutana na Waandishi wa habari na kuazimia kufanya kazi kwa ushirikiano kuhakikisha usalama wa waandishi wa habari wakati wa kutekeleza majukumu yao husussan kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ujao.

Mkutano huo ulifanyika juzi na kuratibiwa na Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC), Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) na kushirikisha wakuu wa polisi wa wilaya za mkoa huo wa kipolisi.

Akizungumza mara baada ya mkutano huo, Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Mtatiro Kitinkwi, alisema wamekubaliana na waandishi wa habari kila mmoja kusimama kwenye nafasi yake wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

"Huu mwaka na ujao kutakuwa na uchaguzi tumejadili namna ulinzi wao utakavyokuwa na nafasi yetu polisi kwenye uchaguzi kwa hiyo tumekumbushana umuhimu wa kutii sheria bila shuruti" alisema.

Alisema mara nyingi waandishi wa habari huwa hawatambuliki wakati jeshi hilo likitekeleza operesheni mbalimbali hivyo wamekubaliana namna bora itakayosaidia kuwatambua ili wawe salama kwenye matukio hayo.

"Kuna wakati tunakuwa na askari ambao hawana sare wakati wa kutekeleza majukumu yetu sasa tumeweka mikakati ya kuhakikisha tunakuwa tunafahamiana kila tunapokwenda kwenye operesheni mbalimbali," alisema.

Alisema ulinzi na usalama ni jambo la msingi ambalo kila mwananchi anajukumu nalo na kwamba katika falsafa ya polisi jamii jeshi hilo litakuwa linatoa taarifa mbalimbali zinazotokea kwenye jamii.

"Tumewaambia kwamba kwa Kanda Maalum ya Dar es Salaam inayounda mikoa mitatu ya Temeke, Ilala na Kinondoni tuna kamishna wa kanda hiyo ambaye ndiye msemaji kwa hiyo taarifa haziwezi kuwa zinatolewa bila kufuata utaratibu ambao jeshi limeuweka," alisema.

Akitoa mada kuhusu ushirikiano wa waandishi wa habari na Jeshi la Polisi, mwanahabari Exuperius Kachenje, alisema takwimu za Baraza la Habari Tanzania (MCT) zinaonyesha waandishi wa habari 272 walikumbwa na madhila mbalimbali wakiwa kazini kuanzia mwaka 2013 mpaka mwaka jana.

Alisema kati ya waandishi hao wanaume walikuwa 219 na wanawake 53 na kwamba madhila mengine yalihusisha waandishi wa habari kushambuliwa mwili wakati wakitimiza majukumu yao.

Kachenje alisema katika kipindi hicho cha miaka 10 matukio 15 ya waandishi wa habari kuharibiwa na kutaifishwa vifaa vyao yaliripotiwa yakiwemo matukio matatu ya mauaji.

MAISHA

Machi 10, 2024
Nipashe


Baba, Mama na Mwan ... pili




# 'JUBA LA RAMADHAN'

Ukurasa 13


**MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA**







| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | J | E | S | H | I |
| S | | | | H | | N |
| T | | B | A | A | | J |
| A | G | A | | B | E | I |
| A | | N | O | A | | N |
| F | | G | | | | I |
| U | K | O | K | O | | A |


## AMSHA AKILI



## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO





Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

EDA, KUU, INA, DAU, RUNGU, IGANA, NYUKA, DAIMA, MAJESHI, UNGUZWA

## WATOTO

# PAKA RANGI




Alichokifanya daktari

WATOTO wawili Juma na John walikuwa wanatembea pembeni ya bustani nzuri ya shule. Wakati wakipiga hatua waliona kipepeo akiruka ruka kwenye maua.Alipomuona kipepeo John alifurahi sana alianza kumuuliza Juma

John: Eti kipepeo ana rangi ngapi?

Juma: Huwezi kuhesabu kwani wapo wengi.

John: Wengi kama kiasi gani?

Juma: Huwezi kukisia kwa sababu ni wengi.

John: Kwa hiyo ukihesabu huwezi kumaliza?

Juma: Kamuulize mwalimu mimi na wewe bado wanafunzi

**SWALI**

Kisiwa cha Pemba kinasifika kwa kilimo cha zao gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mume aenda masomoni, kurudi mkewe mjamzito!

KARIBU tena msomaji wangu. Wiki moja iliyopita niliahidi kukuletea kituko cha jamaa moja aliyekwenda masomoni na aliporejea akamkuta mkewe akiwa na mimba ya mwezi na nusu. Unajua nini kilitokea?

Uaminifu bado ni kitendawili kikali katika nyingi ya familia zetu. Wengi ndoa zimesambaratika kutokana na mmoja wa wanandoa au wote kutokuwa waaminifu.

Anti Flora, yaani wanaume wanasutwa ile mbaya. Lakini ya kwetu mh! Hambongi. Sikia kituko hiki;

"Jamaa yangu kapelekwa kozi India kwa mwaka mmoja na nusu, akamuacha mke na mtoto mmoja. Kabla ya kuondoka alimpeleka mkewe hospitali kujua kama ni mjamzito au la. Nako akaambiwa hakuna kitu, hivyo akaondoka kwa amani.

Anatuma hela kama kawaida. Ulipofikia muda wa kurudi mke alimpokea vizuri sana. Lakini bwana akaona acha akampime tena ili awe na uhakika na afya yake. Alipoenda kumpima akakuta ana mimba ya mwezi na nusu.

Baada ya matokeo hayo, bwana akaona ngoja akamchukue mtoto wake aliyemzaa kabla hawajaoana. Mtoto huyo alipoletwa, huyu mama hamtaki. Bwana kuona vile akampeleka kwa kwa bibi yake.

Bwana akasema kama jeuri yake ndio hiyo, nasubiri mimba hiyo ikue. Wala simgusi kimwili mpaka aone mwisho wake. Sasa anaomba ushauri. Wala bibie huyo hajamwambia mumewe kuwa ana mimba. Tumsaidieje?

Hicho ndicho kituko alichoniletea msomaji wetu. Lakini pia aliunganisha kisa kingine akiomba ushauri na maoni.

Anaanza kwa kusema hivi; 'Hapa tuko kwenye kesi inayotaka kutushinda. Ni hivi, Siku ya Jumapili nyumba ya tatu kutoka ninapoishi kulitokea vurumai ugomvi mkubwa. Mama na baba wamepigana. Bahati mbaya baba kapigwa sana. Kumbe siku zote mke analia wanaamuliwa kesi inaisha.

Sasa mke akagundua mumewe ana nyumba ndogo. Akamtizama yule nyumba ndogo akaona hawezi kumpiga. Mke akamchokoza baba usiku akamwambia; umetoka wapi wewe pepo? Baba akawa mkali kama kawaida ya kinababa.

Akamwambia, unasemaje? Akamnasa kibao. Acha mama ampige. Alikuwa kavaa suruali ya jeans anapiga kumfuu mbaya kabisa. Sasa tatizo wana utajiri. Bwana anamtaka aondoke. Mke akasema hatoki. (msomaji S. Mbuya).

Ama kweli Maisha Ndivyo Yalivyo ndani ya familia zetu. Baba na mama uaminifu kiduchu, watu wazima kudundana bado ni shida kila kukicha. Tufanye nini familia zidumishe amani na upendo? Hebu toa maoni au ushauri kuhusiana na vituko hivyo viwili hapo juu. Kabla sijaondoka sikia ushauri kuhusu kisa cha dereva wa bajaji aliyemruhusu mkewe kwenda kwa wakwe lakini kuondoka tu akazima simu hadi aliporejea. Alipoulizwa kwa nini akaanza kujing'ata ng'ata.

Msomaji wa kwanza anasema; "mimi namuomba huyo kijana waende wote nyumbani kwa wazazi wa mkewe kupata ukweli kama alikuwapo huko kwa siku hizo kumi. Pia amuonye kwa kuzima simu.

Kama hakufika huko, awaombe wazee wamuulize alikuwa wapi. Asisahau kupima ukimwi baada ya siku 90 tangu aliporudi na mwisho achague chuya na mchele. (Msomaji wa Mbeya).

"Ushauri wangu kijana asikurupuke amdadisi taratibu na ikibidi afanye mawasiliano ya huko alikotoka mkewe kusalimia akijifanya kama anawajulia hali.( Diana Eliachim wa Sekei, Arusha).

"Kwa kweli mkasa wa huyo kijana umenikuna lakini namshauri atulize moyo ajaribu kufuatilia nyendo za mkewe huyo kwani hakuna lisilokuwa na ncha na mwisho wa siku atabaini ukweli wa mambo (msomaji Sengerema).

".Anti Flora uliyoeleza ndiyo yaliyomo katika maisha ya kila mwanadunia. Ushauri wangu akubali kutafuta nauli ili waende kwa wazazi akaulize; je, alikwenda au hakwenda ili apate ukweli afanye maamuzi sahihi. Kumbuka vitabu vya Mungu vinasema usiishi na mwanandoa msaliti. (Ibrahim Kinyaga wa Iringa).

"Inawezekana kazi ya huyo bwana inampunguzia ukaribu na mkewe, saa nyingi yupo kazini hadi usiku mwingi. Mwambie ajichunguze? (msomaji).

"Kwa ushauri wangu kijana huyo apunguze jazba, kisha afanye uchunguzi nyumbani kwa wakwe kwa kuwapigia simu kuwauliza kama binti alifika salama na kadhalika. (Emmanuel Mngano, Morogoro).

***"Tatizo siku hizi maisha na hasa mapenzi yamekuwa rahisi mtu anapanga tu wapenzi kuanzia nyumbani alipozaliwa, gengeni, dukani, shuleni, kazini na kadhalika. Uaminifu kitendawili kikubwa! (Justine Mtasiiwa wa Dar). Je, una maoni, ushauri? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Yaishi maono yako, mengine ni kupoteza talanta

UKIONA mtu anatumia nguvu kubwa sana kukufanyia majungu, kukuchafua kutaka uharibikiwe kimaisha na kukuondoa katika eneo ulilopo, usishangae!

Elewa kwamba huyo ni mmoja wa wale wanaotegemea kuishi ndoto au maono ya wengine.

Kufanya hivyo anadhani kwamba yeye ndiye anastahili kuwapo katika nafasi uliyo nayo. Ni wale wanaotamani mafanikio ya wenzao badala ya kuvutiwa nayo.

Ikitokea umekutana na mtu wa namna hii, usigombane naye wala usimchukie. Tambua siku zote kwamba, mtu wa namna hiyo yupo gizani na wewe ni nuru.

Hakuna namna hata mara moja giza likaizidi nuru. Endelea kusimamia unachoamini na hasa ukimtambua aliyekubebesha maono hayo ni Mungu, hivyo yatatimia tu. Ni suala la muda.

Katika Biblia, tunasoma kwamba Bikira Mariam, mama wa Yesu Kristo, alimtambua aliyembebesha maono. Hakusita kuipokea baraka ile wala hakujali kama mchumba wake, Yusufu angemwacha.

Wala hakujali jamii inayomzunguka itasema nini juu yake. Alisimamia alichokiamini na aliyemwamini (Mungu) aliyembebesha maono yale.

Kwa nini nimeanza ujumbe huu? Nataka kuwatia moyo wanawake, dada zangu, mama zangu na wanangu wa kike wasiache maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ikapita bila kutafakari haya. Kubwa ni kukaa na kutafakari nafasi yako kwenye jamii, ni jambo gani umelifanya.

Siku ya Wanawake Duniani ilianzishwa kwa sababu nyingi na za msingi. Ukiangalia kwa ujumla linazungumza sana suala la mifumo ndani ya jamii, mifumo dume, mifumo ambayo inaacha kundi moja, inapeleka kundi lingine mbele.

Msisherehekee na kuimba nyimbo kwenye majukwaa, kumbi za starehe na viwanja mbalimbali. Kaeni tena chini na mtafakari mustakabali wa maisha yenu katika maendeleo ya familia, maendeleo ya taifa na haki zenu za msingi ndani ya taifa hili mnazipataje.

Mwaka huu wa 2024, kauli mbiu yenu inasema, 'wekeza kwa mwanamke kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii.'

Na upungufu huo ndiyo haya tunayosema yanatokana na mifumo, taratibu, mitizamo iliyojengeka ndani ya jamii na imani, zimeona kwamba huyu labda hawezi kufanya hiki na haruhusiwi kufanya hiki.

Matokeo yake mnajikuta mko hatua kadhaa nyuma na wenzetu wanaume wako hatua kadhaa mbele yenu. Jambo moja ambalo ni la kimfumo, mnapaswa kuliwekea nguvu ya pamoja ni lile linalomuondoa mwanamke kwenye wigo wa meza ya maamuzi.

Wanawake kutokushiriki vizuri kwenye meza ya uamuzi ni changamoto kubwa sana ambayo mambo mengi yanayoamuliwa kule. Kuna mambo ya sera, kuna mambo ya rasilimali, kuna mambo mengi yanayoamuliwa katika mchakato mzima wa sera.

Keki imewekwa mezani, wanaokata ni wengine wewe uliyeko jikoni unategemea uletewe kipande cha namna gani? utaletewa makombo au watakusahau kabisa?

Ni lazima muangalie ni ipi nafasi ya mwanamke katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji, ambao unatarajiwa kuufanya baadae mwezi Oktoba mwaka huu.

Ni lazima mwanamke, atambue nafasi yake ina nguvu sana ya kugusa mfumo uliowavuta nyuma, uliowaweka mateka kwa kipindi cha zaidi ya miaka na karne katika maisha yenu.

Wekeni nguvu ya kuangalia uchaguzi wa serikali za mitaa kwenye yale maeneo ya kuchaguliwa na siyo ya viti maalum. Ongezeni zaidi idadi ya wanawake kwenye maeneo ya uchaguzi.

Pamoja na kwamba, ni sera ambayo imewasaidia sana lakini sasa hivi mnapaswa kuwa na jicho la ziada. Kwamba asilimia 50 kwa 50 mliyoitaka inakuwa yenye sauti.

Niwape mfano mmoja, kuna wenzenu wa serikali ya Rwanda. Rwanda sasa hivi wanawake katika uongozi wako zaidi ya asilimia 60.

Ukiangalia huku kwetu Tanzania, mwanamke akishaingia Bungeni hataki kutoka, anaingia kipindi cha kwanza, atakaa kipindi cha pili, cha tatu, anang'ang'ania huko na bado anaendelea kupigiwa kura.

Wanawake ambao ni wenyeviti wa vijiji kwa Tanzania nzima, ni asilimia 2.9 lakini ukiangalia kwenye vitongoji, ni asilimia 6.7 ambao ni wenyeviti. Idadi iliyobakia yote ni wanaume karibu asilimia 90.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***







Septemba 10, 2023 ilikuwa siku ya kukumbukwa kwa Boniphace Bwire Mateko na Regina Mbwambo Msifuni baada ya kufunga ndoa katika Kanisa la Wasabato Bomani mjini Bunda mkoani Mara. Sherehe ya kuwapongeza ilifanyika katika ukumbi wa Malaika Resort.





# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

## PICHICHI TURBAN-1

# Mbunifu wa 'Juba la Ramadhan'









UMAARUFU wa mavazi ya Stara umeongezeka nchini na hata duniani kote, hivyo kuwafanya wabunifu kama Pichichi kufikiria nje ya boksi.

Hapa Nchini umaarufu wa vazi hili umetokana na harakati nyingi yakiwemo majukwaa kama Stara Fashion Week. ambalo hufanyika kila mwaka .

Rais Samia Suluhu Hassan anatajwa na wasanii kuwa mmoja wa alama ya mitindo, katika mavazi haya baada ya kuonekana katika shughuli mbalimbali za kiserikali kama kiongozi mkuu wa nchi au hata anaposafiri nje ya nchi katika ziara za kikazi.

Kiongozi huyu aliyeingia madarakani Machi 19, 2021 amekuwa rais wa kwanza mwanamke nchini, na anaonekana akipendeza na mavazi yaliyotengenezwa kwa mitindo mbalimbali na hivyo kubeba utambulisho wake.

Katika wabunifu wanaomuangalia kwa jicho la karibu, Said Ndee maarufu Pichichi Turban ambaye aliwahi kubuni vazi la Royal Tour akihamasisha na kuunga mkono juhudi za kitaalii nchini kwa mavazi ya stara, amesema anamuangalia rais kama kioo cha hamasa kwenye kazi zake.

Wakati huu wa mwezi mtukufu wa ramadhani, mbunifu huyo amekuja na vazi la stara ambalo amelipa jina la juba la ramadhani , akichanganya tamaduni za kimasai katika vazi hilo ambalo limezinduliwa siku chache kabla ya mwezi mtukufu wa ramadhani.

Safari ya ubunifu ya Pichichi ilianzia mwaka 2019 alipobuni kilemba kilichompa umaarufu mkubwa kariakoo.

Kwa mujibu wa Ndee, wakati huo alikuwa na uelewa kidogo wa masuala ya ubunifu.

Anasema alihangaika na michoro kadhaa ili kupata ulio bora, ndipo akafanikiwa kuupata mchoro wa kofia aliyoletewa na rafiki yake kutoka China sasa ikawa kazi kumpata fundi ambaye ataweza kushona kama ambavyo inatakiwa kuwa.

Saidi anasema kupata kilemba cha kwanza na kukitumia kama mfano, alimruhusu akashone dazeni 20 za vilemba hivyo na vilemba 50 kwa ajili ya soko la Kariakoo.

Anasema alifanikiwa kushona vitambaa hivyo na kumpelekea na kwa mara ya kwanza anaanza kupata mwangaza katika macho yake baada ya kuambiwa kilemba kile kimeuzika vizuri sokoni na kiliisha chote.

Kufanya vizuri kwa kilemba cha kwanza, ndipo alipopata wazo la kubuni kilemba cha pili ili kujitafutia ajira yake binafsi kupitia sanaa hiyo ya ubunifu.

Anasema ilibidi kujifungia ndani mwenyewe, akabuni kilemba kofia kingine alichokipa jina 'mwendokasi' ambapo hii aliongeza mauzo na kumfanya rafiki yake afurahie uwepo wake katika biashara hiyo.

ITAENDELEA JUMAPILI

UREMBO

Na Mary Geofrey

# NGOZI YA USO

## Hung'arishwa kwa vitu asili



UZURI wa ngozi sio rangi tu bali ni mwonekano wenye afya na mng'ao unaoashiria maisha mazuri.

Katika kuhakikisha unakuwa na ngozi nzuri na yenye afya, leo tutaelekezana namna ya kutunza ngozi kwa njia ya asili ya kutumia kiini cha yai, machicha ya nazi, tango na limao.

Utunzaji wa aina hii unaweza kufanya mara moja kila baada ya wiki mbili au mara moja kwa mwezi.

JINSI YA KUFANYA

Andaa maji safi yenye joto kiasi yanayohimili ngozi yako.

Kwa kutumia maji hayo osha uso taratibu, kama una ngozi kavu au ya kati chukua kipande cha tango kidogo na upake maji yake usoni.

Wenye ngozi ya mafuta unaweza kutumia kipande cha limao kwa kupaka maji yake.

Chukua pamba au kitambaa laini na futa maji ya matunda usoni kwa mtindo wa kusafisha taratibu usoni.

Kisha chukua machicha ya nazi na anza kuusugua uso na shingo taratibu hadi uridhike kama umepitiwa kikamilifu. Utagundua hilo pale utakapoona unang'aa kwa mafuta yaliyotoka kwenye nazi.


Kisha ondoa machicha usoni ili kuacha ukiwa na mng'ao.

Chukua kiini cha yai inapendeza ukitumia la kienyeji au la kisasa lenye kiini cha njano iliyokolea.

Paka ute mzito wa njano wa kiini uso mzima bila kusahau shingoni na nyuma ya masikio.

Baada ya kupaka kiini cha yai endelea na shughuli zako huku ute wa yai ukiendelea kukauka. Ikikauka ngozi yako inakuwa kama inajivuta.

Hakikisha unaosha uso wako kwa maji safi ya baridi.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mboga ya kabichi na mayai

KABICHI ni aina ya mboga za majani ambayo hupikwa kwa mapishi tofauti.

Unaweza kupika kabichi yenyewe bila kuchanganya na chochote, pia unaweza kupika kwa kuchanganya na nyama, mayai au chochote unachoona kinafaa kuwa mboga.

Leo tutaangalia jinsi ya kupika kabichi iliyochanganywa na mayai.

**MAHITAJI**

Kabichi moja ya ukubwa wa wastani, mayai manne, mafuta robo lita, vitunguu vinne, karoti kubwa moja, pilipili manga kiasi, chumvi kiasi kwa ladha na mafuta ya kupikia.

**JINSI YA KUPIKA**

Chukua kabichi ulikatekate kisha ulioshe, washa jiko lolote ulilonalo liwe la mkaa, gesi au umeme.

Kisha bandika kabichi ulilolikatakata na kuliosha liache liive kidogo kisha ipua.

Menya nyanya, katakata vitunguu, karoti uviweke tayari kwa mapishi.

Bandika sufuria jikoni na utie mafuta ya kupikia, yakipata moto tia vitunguu ukaange mpaka vibadilike rangi kisha tia nyanya ukaange.


Nyanya zikishaiva tia karoti kaanga kidogo na baada ya hapo tia pilipili manga pamoja na kabichi ulilolichemsha.

Vunja mayai uliyoandaa na kisha changanya na kabichi lililoungwa tayari na ukoroge hadi mboga yako ikauke.

Mboga yetu ya kabichi iliyochanganywa na mayai itakuwa imeiva na tayari kwa kuliwa kwa chakula ukipendacho iwe ugali, wali au hata pilau.



## Kijumba binafsi ni kivuli murua



**Na Restuta James**

KUWA na bustani yenye kivuli na mazingira tulivu nyumbani kwa gharama nafuu ni jambo linalohitaji ubunifu wa hali ya juu. Hata hivyo, jambo hilo limerahisishwa kutokana na namna ambavyo matumizi ya teknolojia na upatikanaji wa habari unavyotoa nafasi ya kujifunza kutoka kwa wabunifu na wataalamu wa nyumba kwa urahisi kabisa.

Ipo mitandao na tovuti mbalimbali zinazotoa fursa ya watu kuona kazi za maboresho ya nyumba kuanzia ujenzi hadi ukamilishaji na mazingira yake.

Mbunifu wa bustani, Diana Mwaikambo, anasema kijumba binafsi kina faida nyingi ikiwamo kupamba bustani au eneo la nyumba, kwa kuhakikisha kivuli kipo muda wote na hivyo kuwa na mazingira ya kupumzika kila wakati.

Anasema kijumba hicho ni kizuri kwa ajili ya mazungumzo ya familia na hasa siku za mapumziko kupata chakula pamoja au kinywaji.

"Ni sehemu inayoweka kumbukumbu za kifamilia na ni eneo zuri sana kukaa na mgeni. Ukiwa na kivuli cha aina hii, hutotamani kutoka nyumbani, naona kila mwenye nyumba anafaa awe nacho," anasema Diana.

Diana anasema aina hii ya vivuli, inatengenezwa kwa chuma na mbao au mojawapo ya zana hizo, ikiezekwa kwa bati au makuti; kulingana na pendekezo la mwenye nyumba.

Anashauri kwamba pamoja na wataalamu kama yeye kuwapo nchini, mtu anayehitaji kujenga kijumba hicho, anaweza kutafuta mtandaoni na kujionea aina mbalimbali kabla hajafanya maamuzi ya ujenzi.

"Bando na muda wako ndiyo tiketi ya kukufikisha kwa wabunifu walio nje ya Tanzania na bara la Afrika, ambao wanatoa mbinu za kila aina kulingana na bajeti yako. Nawashauri Watanzania wenzangu wasiwe wavivu, watumie mitandao ya kijamii kwa faida," anasema.

**DONDOO MUHIMU**

- Kinapendeza kikijengwa kwa mbao
- Panda maua machache kukizunguka
- Unaweza kuweka mapazia, mlango sio lazima
- Fenicha za nje za asilia ni nzuri zaidi

**Na Elizabeth Zaya**



# HIVI NDIVYO NYUMBA YA KUFUGIA MBWA INAVYOTAKIWA KUWA

NYUMBA ni mojawapo ya jambo muhimu sana katika maisha ya binadamu iwe ni ya kupanga au ni ya kumiliki mwenyewe.

Kutokana na umuhimu wa nyumba hiyo na ili iendelee kustawi kwa kuwa msaada zaidi, inahitaji kujengwa kwa viwango bora ili isiharibike haraka na iwe rafiki wa mazingira.

Inahitaji matunzo ikiwamo kufanyiwa usafi na kukarabatiwa pale inapohitajika kufanyiwa hivyo.

Kama ilivyo katika ujenzi bora kwa nyumba ya binadamu, kadhalika na kwa wanyama, nao baadhi wanahitaji kuishi katika nyumba ili kulinda ustawi wao.

Mtaalam wa kufuga mbwa, Richard Chacha, anasema mbwa wanaofugwa kwa ubora wanatakiwa kufugiwa katika nyumba maalum.

Anasema nyumba ya mbwa mara nyingi zinatakiwa ziwe ndani ya uzio wa nyumba ya mfugaji mwenyewe kwa sababu pia anahitaji uangalizi na kuepusha hatari ya kudhuru watu.

"Ufugaji wa mbwa ni jambo jema kwa sababu lengo lake ni kuimarisha ulinzi katika nyumba. Badala ya kutumia au kuajiri walinzi katika suala la usalama, ukiwa umefuga mbwa inasaidia zaidi. Mbwa ana faida nyingine kwa sababu akiwa amefugwa vizuri na kufundishwa ni rahisi kubaini wahalifu kwa sababu mbali na kupambana nao, hutoa kelele za tahadhari," anasema Chacha.

Anasema ili ufurahie kuwa na nyumba bora, lazima pia umjengee makazi bora ili awe na afya njema.

Chacha anasema baadhi ya vitu muhimu ambavyo unapaswa kuzingatia wakati wa ujenzi wa nyumba ya mbwa ni pamoja kuhakikisha nyumba yake inakuwa na nafasi ya kutosha ambayo itamuwezesha kujigeuza kwa kadri anavyohitaji.

Anasema nyumba ya mbwa inapaswa kuezekwa kama kawaida japokuwa siyo lazima iwe bati. Pia anasema lazima iwe na mwanga wa kutosha badala ya giza ili kumwezesha kufanya shughuli zake za ndani kwa ndani.

Jambo lingine anasema lazima uhakikishe nyumba inakuwa na sehemu za uwazi wa wastani wa kupitishia hewa.

Mbali na hilo, anasema lazima iwe na mlango na kufuli ambao utakuwezesha kumpitishia wakati wa kumfungulia kwa ajili ya ulinzi na pia wakati anarudi ndani.

Pia anasema lazima kuwekwe na sehemu nzuri ndani ya nyumba hiyo ya mbwa ambayo itatumika kumtengea chakula ambayo itamwezesha kula kwa uhuru.

Chacha anasema pia lazima uhakikishe kwamba unamwekea kifaa maalum ndani ya nyumba yake ambacho kitatumika kuhifadhia maji yake ya kunywa.

Anasema pia nyumba ya mbwa inahitaji kufanyiwa usafi kama ilivyo nyumba ya binadamu, na kuna umuhimu wa kuhakikisha usafi huo unafanywa mara kwa mara ili kumuepusha na maradhi.

Chacha anasema kwa kuwa nyumba ya mbwa hujengwa ndani ya uzio wa nyumba ya kuishi binadamu, ni lazima suala la eneo la kujengewa nyumba hiyo ya mbwa lizingatiwe.

"Tunajua kwamba nyumba za mbwa kwa kawaida huwa siyo kubwa, na wengi wetu hupendelea kujenga au kuezeka na vitu vya ajabu ajabu ambavyo wakati mwingine inaweza kusababisha kuharibu muonekano mzuri na madhari ya nyumba, pia kama unaona itaharibu ni vema ujenge ambayo unaweza kuihamisha.


"Unaweza kuingia katika baadhi ya makazi ya watu, wanakuwa na nyumba nzuri, lakini unakuta hapo katikati ya nyumba wamejengea kibanda cha mbwa kibaya hadi kimeharibu kabisa 'fashion' ya nyumba. Kwa hiyo siyo vibaya kuchagua eneo zuri la kuweka vibanda hivyo," anasema.

Anasema nyumba ya mbwa pia inaweza kupakwa rangi kama zinazotumika kupaka katika nyumba wanazoishi binadamu.

"Kama unathamini kazi kubwa ya ulinzi inayofanywa na mbwa wako nyumbani, lazima pia uthamini maisha yake na makazi yake. Ikiwezekana paka rangi ya nyumba yake, weka hata vyombo na chakula bora kwenye nyumbayake na hii itasaidia awe na afya bora," anasema Chacha.



# KATUNI


JUKWAANI
KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
LOH!
WA MITAANI
OFISI YAKO SIONI MANUFAA YAKE UMEKALIA KITI TU! 'NAUNYWEA POMBE' MSHAHARA WANGU WALA SIKEMEWI!
UKIPOKEA TENA NIITE
MWENE-KITI WA MTAA
UKATILI
ONA SASA! NIMEKWAMBIA WESE TUSILIJAZE 'FULU TANKI' WEWE MBISHI!
MI'MWENYEWE NIMETEPETA! LAKINI WEWE NDIO UMETAKA 'TUPIGWE CHINI' KONDA UNAIBA MPAKA HESABU YA BOSI
SINA SHAKA POMBE ZA VUNJA' JUNGU SIO ZA KUZIENDEKEZA UNAWEZA KUWEHUKA UKIWA NA AKILI TIMAMU!!!
ASIBISHE NIMEMSIKIA AKIMWAMBIA MWANAMKE WAKAVUNJE JUNGU!
UTUERESE KWA UWASI TUKUEREWE HIRO JUNGU MMIRIKI WAKE MUNAMJUA?
POSTI
WE'AFANDE NAONA BORA UTUPISHE KAPUNGE UPEPO NJE!
NIMESAHAU TESTA IPO JUU YA MEZA NENDA KANILETEE
ACHA WOGA TESTA NI WEWE GUSA WAYA
SIO MAISHA TU HATA SIKIO UNATOBOA....

## HABARI KIMATAIFA

# Haiti inaelekea kuanguka, wafungwa 3,000 watoroka

**PORT-AU-PRINCE,** HAITI

WAKATI ghasia zikiongezeka nchini Haiti, kiongozi wa mapinduzi ya 2004, Guy Philippe, amejitokeza na kumtaka Waziri Mkuu, Ariel Henry, kujiuzulu.

Philippe, ambaye alirejea nchini Haiti mwaka jana baada ya kutumikia kifungo nchini Marekani, aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba anataka kuwa rais.

Mpaka sasa shughuli katika mji mkuu wa Port-au-Prince, zimezorota kutokana na kuenea kwa ghasia zinazofanywa na magenge ya kihalifu.

Waziri Mkuu, Henry alishindwa kurudi nchini humo baada ya kwenda nchini Kenya kuhudhuria mkutano wa kujadili kusaidiwa vikosi vya polisi watakaokwenda kulinda amani.

Philippe, ambaye alifukuzwa nchini Haiti mnamo Novemba baada ya kutumikia kifungo cha miaka sita jela kwa makosa ya kula njama ya kutakatisha pesa za dawa za kulevya, alisema Henry anapaswa kujiuzulu na kuwaacha Wahaiti waamue hatima yao. Alipoulizwa kama alitaka kuwa rais, alikubali na kueleza anataka kuingia katika ulingo wa siasa.

"Nilikuwa seneta, nimechaguliwa na watu wangu, nitaingia tena katika uchaguzi," alisema Philippe, ambaye alikuwa mmoja wa viongozi wakuu katika mapinduzi ya 2004 yaliyomuingiza madarakani Rais Jean-Bertrand Aristide.

Wakati huo huo, jumla ya wanawake wajawazito 3,000 nchini humo wanakabiliwa na kitisho cha ukosefu wa huduma baada ya sekta ya afya kupagaranyika.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa nchini Haiti, ilionya juzi kwamba karibu wanawake 450, huenda wakakabiliwa na matatizo ya uzazi na kutishia maisha ikiwa hawatapokea msaada wa matibabu.

Mgogoro wa Haiti umeibua wasiwasi kutoka kwa nchi ya Marekani ambayo imemtaka waziri mkuu wa nchi hiyo ambaye yuko uhamishoni nchi jirani, kufanya mageuzi ya haraka ya kisiasa ili kuzuia kuongezeka kwa ghasia.

Makundi ya wahalifu, ambayo tayari yanadhibiti sehemu kubwa ya mji mkuu pamoja na barabara zinazoelekea katika maeneo mengine ya nchi, yameshambulia miundombinu muhimu ikiwa pamoja na magereza mawili na kuruhusu wafungwa zaidi ya 3,000 kutoroka.

**DW**



Magari ya jeshi la Nigeria yakiwa katika eneo la shule waliyotekwa wanafunzi kaskazini magharibi mwa Nigeria juzi. **PICHA: AP**

# Meghan alalamikia ubaguzi na unyanyasaji

**TEXAS,** MAREKANI

MEGHAN Markle ambaye ni mke wa mwanamfalme wa Uingereza, Harry, ameikosoa baadhi ya mitandao ya kijamii kwa kueleza imekuwa ikimlenga kwa uonevu na unyanyasaji unaotokana na ubaguzi. Alisema mitandao hiyo inatumika kujaza sumu inayoonekana kutokuwa na mwisho dhidhi yake.

Meghan alikuwa mzungumzaji mkuu kwenye jopo la hadhi ya juu katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake kwenye tamasha la kila mwaka la SXSW linalofanyika Austin, Texas nchini Marekani.

Alisema kwa sasa ameamua kujitenga na mitandao kwa ustawi wake na watoto.

Katika mahojiano hayo, mwanamfalme Harry alikuwa mstari wa mbele wa watazamaji waliohuhudia hafla hiyo.

Meghan alisema watu wamesahau ubinadamu katika baadhi ya vyombo vya habari na nyanja ya dijitali.

"Sehemu kubwa ya uonevu na unyanyasaji niliokuwa nikipata kwenye mitandao ya kijamii wakati nilikuwa na ujauzito wa Archie na Lili", alieleza. "Unafikiria tu juu ya hilo na kujiuliza kwa nini watu wawe na chuki kiasi hicho, hili sio nia mbaya tu ni ukatili." Aliongeza.

**BBC**

# Marekani yadai raia wake kunyanyaswa Zimbabwe

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeishutumu Zimbabwe kwa kuwanyanyasa, kuwaweka kizuizini na kuwafukuza raia wake kadhaa waliokuwa nchini humo kama wafanyakazi wa misaada.

Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) lilisema maofisa wa serikali na wakandarasi walikuwa wametishwa kwa maneno na kimwili.

Shirika hilo lilisema kwamba eaia hao walikuwepo nchini humo kuunga mkono ushiriki wa raia, taasisi za kidemokrasia na haki za binadamu.

Ilisema kwamba dhamira ya Zimbabwe katika mageuzi ya kidemokrasia ilikuwa sawa na sifuri. Serikali ya Zimbabwe bado haijasema chochote kuhusu madai hayo ya USAID.

Siku ya Jumatatu, Marekani ilitangaza vikwazo vipya kwa Rais wa Zimbabwe Emmerson Mnangagwa na maofisa wengine wakuu wa serikali, ambao inawatuhumu kwa rushwa na ukiukaji wa haki za binadamu.

Vikwazo hivi vilibadilisha vikwazo vilivyowekwa miongo miwili iliyopita.

Msemaji wa Rais Mnangagwa alilaani vikwazo hivyo na kusema kuwa ni vitendo vya "uadui" na kuishutumu serikali ya Marekani kwa "kashfa zisizo na maana".

# Rais apatikana na hatia biashara dawa ya kulevya

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Honduras, Juan Orlando Hernandez, amepatikana na hatia katika kesi inayomkabili ya ulanguzi wa dawa za kulevya.

Kiongozi huyo amefunguliwa mashtaka katika mahakama ya shirikisho nchini Marekani.

Hernandez alipatikana na hatia hiyo Ijumaa, baada ya hakimu kueleza anahusika kula njama ya kuingiza dawa za kulevya aina ya cocaine nchini Marekani, na kumiliki vifaa vinavyosababisha uharibifu ikiwamo bunduki.

Waendesha mashtaka walisema rais huyo wa zamani aliendesha serikali nchini Honduras kama jimbo la madawa ya kulevya, ikiwa ni kuwalinda na kupokea hongo kutoka kwa walanguzi wa dawa hizo.

Kutokana na uamuzi huo, Hernandez anakabiliwa na hukumu ya kifungo cha maisha jela.

Rais huyo wa zamani mwenye umri wa miaka 55 alikana makosa yote na kueleza hana hatia katika kesi hiyo.

Kiongozi huyo alitiwa hatiani na jopo la majaji wa mahakama ya shirikisho ya Manhattan baada ya kusikilizwa kwa siku mbili.

Hernandez alikuwa rais wa Honduras kutoka 2014 hadi 2022, akihudumu kwa mihula miwili mfululizo.

Waendesha mashtaka walimshtumu kwa kushirikiana na baadhi ya walanguzi wakubwa wa mihadarati duniani ili kujenga himaya mbovu, yenye jeuri na kikatili kwa kunufaika na usafirishaji haramu wa tani za kokeini kwenda Marekani.

Miezi mitatu baada ya kuondoka madarakani, alirejeshwa nchini Marekani na alikamatwa Aprili 2022, kujibu mashtaka katika mahakama ya shirikisho.

Wakati wa uongozi wake, Hernandez mara moja alionekana kama mshirika mwenye nguvu wa Marekani na ilikuwa ikipokea zaidi ya dola milioni 50 kama msaada wa kusaidia kupambana na dawa za kulevya.

Mnamo 2019, Rais wa wakati huo Donald Trump alimshukuru Hernandez kwa kufanya kazi kwa karibu na Marekani.

**BBC**

SAFU

MAKALA

# TUWALEE WATULEE



Na Magabilo Masambu

**Hakuna mtoto anaweza kurithi kazi ya baba yake bali anaweza kujifunza na akafanya kazi ya baba yake hasa tunapowaaminisha watoto wetu kwamba hakuna haja ya kupata shida kwa kuwa baba yenu ninazo pesa za kutosha. Tunawafanya watoto wasifikirie zaidi kujenga maisha yao wenyewe na kubaki kutegemea maisha ya wazazi wao na pindi wazazi wanapofariki dunia, wanabaki kwenye migogoro mikubwa.**

MAISHA ya watoto huanza na malezi kwa maana kwamba ni muhimu zaidi wazazi na walezi kuwalea katika misingi yenye maadili mema na mazuri kama ambavyo vitabu vyote vitakatifu vinatufundisha.

Msingi wa malezi bora huanza ngazi ya familia.

Watoto hujifunza mambo mengi kutoka kwa wazazi na ndugu wa karibu wanaowazunguka, hivyo ili watoto wajifunze maadili mema, ni lazima sisi wenyewe tuwe na maadili mema ili iwe rahisi kwa watoto kujifunza tabia njema kutoka kwetu.

Changamoto kubwa kwa sasa ni juu ya utandawazi jambo linaloonekana kuharibu maadili kwa sababu dunia sasa imekuwa kama Kijiji, hivyo kuwa ngumu kudhibiti mwingiliano wa mila na desturi mbalimbali ambazo zinaweza kuwa chanzo cha maadili mabaya au maadili mazuri kutegemeana na mambo gani tunajifunza.

Tunaweza kujenga au kuandaa maisha ya watoto wetu kupitia elimu kwa maana ya mfumo rasmi au usio rasmi.

Kwa miongo kadhaa, tumekuwa tunaamini kwamba ili ufanikiwe lazima usome na pengine ni kweli kwa kuwa tunawaona wengi waliosoma wamefanikiwa katika maisha hasa tunapowatazama viongozi wetu.

Wengi wamesoma, hivyo kuendelea kutufanya tuamini kwamba tukisoma tutafanikiwa, hata maandiko yanasema "mkamate sana elimu, usimwache aende zake, mshike maana yeye ni uzima wako" kwa hiyo ni muhimu sana kuhakikisha tunawapatia watoto wetu elimu itakayowasaidia kutatua changamoto za maisha watakapohitaji kujitegemea.

Tuwapeleke watoto shuleni wasome ili baadaye wajiajiri au kuajiriwa na hatimaye kujikimu kimaisha kutokana na ujira wa kazi ambazo watakuwa wakizifanya. Kwa njia hiyo, tutakuwa tumewajengea msingi mzuri wa maisha yao na elimu.

Hapa inajumuisha elimu ya vitendo ambayo pia inawasaidia sana watoto wasioweza elimu ya nadharia, hivyo tuwawekee mkazo mkubwa katika elimu ya ufundi ambayo kimsingi hutengeneza mamilioni ya ajira binafsi kuliko kusoma nadharia na kusubiri kuajiriwa.

Stadi za maisha, nje ya elimu na mambo mengine tunawajibika kuwafundisha pia kwa sababu maisha hayana njia moja ili kuyafanikisha, hivyo ni muhimu watoto wetu kupata elimu nyinginezo zitakazowafanya kujitegemea baadaye.

Mfano, kazi za nyumbani kama kupika, kufagia, kufua nguo na kulima tukizingatia kwamba kilimo pia ni njia mojawapo inayoweza kuwafanya wakajikimu kimaisha baadaye na ususi, ni shughuli zitakazowafanya wajitegemee vizuri kuliko kufikiria tu kwamba kila mtu lazima asome na aajiriwe

Eneo lingine muhimu ni uhusiano. Tunapojenga utu na ustaarabu wa watoto wetu tuwafundishe kuthamini watu wengine kama wanavyojithamini. Tuwafundishe wawe na uhusiano mwema kwa jamii na ndugu zao. Ikiwa wazazi au walezi watafariki dunia, basi watoto hawa watabaki na kuishi vizuri na watu wengine hasa kulingana na utamaduni wa kiafrika.

Ni muhimu sana kujenga uhusiano vizuri na hili litasaidia watoto wetu kuwa raia wema katika nchi kwa sababu wakishatambua umuhimu wa watu wengine kwenye maisha yao, hawatawatendea wengine mabaya, hivyo watakuwa raia wema, wanaowapenda wengine.

Jambo hili litawezekana tu kama wazazi tunayaishi maisha ya namna hiyo ili tutakachokuwa tukikihubiri kwa watoto wetu tuwe mfano na kuwarahisishia kuelewa haraka zaidi.

Hakuna mtoto anaweza kurithi kazi ya baba yake bali anaweza kujifunza na akafanya kazi ya baba yake hasa tunapowaaminisha watoto wetu kwamba hakuna haja ya kupata shida kwa kuwa baba yenu ninazo pesa za kutosha.

Tunawafanya watoto wasifikirie zaidi kujenga maisha yao wenyewe na kubaki kutegemea maisha ya wazazi wao na pindi wazazi wanapofariki dunia, wanabaki kwenye migogoro mikubwa.

Kama hawakuandaliwa watapigana na kuuana sababu ya mali za wazazi, hivyo ni muhimu kuwajenga watoto katika dhana itakayowafanya wasibweteke na kufikiri kwamba hawana haja ya kutafuta maisha yao wenyewe kwa kuwa wazazi wana maisha mazuri. Wengi wao tumeona wanavurugana na hata kuuana baada ya wazazi kufariki dunia.

Unapowasomesha watoto ni kuwatengenezea maisha yao binafsi ya baadaye.

Kama atasoma, faida ya kwanza ni yeye mwenyewe kujitegemea na kujikimu na mahitaji yake ya kila siku na familia yake kama atakuwa nayo.

Nasema hivyo kwa sababu naye atakuwa mzazi atakayekuwa anategemewa kama ambavyo nasi kwa sasa tunategemewa na watoto wetu.

Pili, ni mzazi au mlezi kujiandalia maisha yake ya baadaye atakapokuwa mzee. Hapa wazazi au walezi wengi hawalijui hili kutokana na uchumi wa nchi zetu.

Ni vigumu sana serikali zetu za kiafrika kuweka utaratibu wa kuwalea wazee, hivyo kusababisha kulelewa na watoto wao wa kuzaa au wanaowalea na wanapozeeka hulelewa na watoto hao. Unapokuwa unafanya kazi na bahati nzuri una pesa za kutosha, wakati mwingine unapofushwa na kazi au na fedha na kushindwa kuona mbele kwamba siku ukizeeka unahitaji msaada wa watoto wakulee.

Tunawajibika kwa namna yoyote ile, kuandaa maisha ya watoto wetu au wale tunaowalea ili kutengeneza njia nzuri itakayokuwa na msaada kwa kila mmoja kwa wao binafsi au sisi wenyewe kama wazazi, kwa jamii na kwa taifa kwa ujumla kwani familia bora hujenga taifa bora. Hatuwezi kuwa na viongozi bora kama hatuna familia bora inayowajali Watoto.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Nikila unasema, nikinunua nguo unasimanga, nikijipodoa unacheka*



Na Adam Fungamwango

**"Safiri salama kawasalimie wote na ukifika salama urudishe majibu mapema. Salamu sana kwa baba, salamu sana kwa mama, uwaeleze sijambo, bali nimekonda kwa gubu la mume. Hakuna kitu ninachokosa humu nyumbani, kama ni nguo ninavaa za kila aina, toka vitenge mpaka khanga hazinipiti, ila gubu tu la mume."**

JUZI, wanawake wote duniani walikuwa wanaadhimisha siku yao. Tumeona wakifanya mambo mbalimbali ya kijamii wenyewe binafsi au kwa kungana pamoja kwenye taasisi wanazofanyia kazi au kuzitumikia.

Leo tunajikita kuhusu madhila na changamoto mbalimbali wanazopitia kwenye jamii, likiwemo suala la uhusiano.

Ni kweli wanaume nao huwa wanalalamika kuwa wanapitia wakati mgumu wanapokuwa kwenye uhusiano lakini wanawake kunapotokea matatizo kwenye ndoa au uhusiano, ndio wanaoathirika zaidi. Mara nyingi wanawake ni wavumilivu sana, lakini inafikia sehemu yakizidi uvumilivu unawashinda.

Ni mwanamke tu ndiye anayeweza kuishi na mwanaume mlevi, mvuta sigara, mwongo, mwizi, mwenye tabia ya kupiga, gubu na hila nyingi tofauti. Kama hila hizo anakuwa nazo mwanamke, sidhani kama kuna mwanamume angekubali kukaa na mtu huyo.

Nawaletea hadithi ya mama mmoja ambaye alikuwa na mwanamume mwenye gubu. Anaongea sana huyu mwanamume. Akirudi usiku mwanamke halali, maneno mpaka kunakucha.

Ukiacha hilo, anamtunza vizuri tu mkewe kwa nguo, chakula na kila kitu lakini mwanamke analalamika gubu.

Anatembelewa na ndugu yake anayekaa hapo kwa siku kadhaa na wakati anaondoka, mwanamke anamtuma apeleke salamu kwa wazazi wake kijiji kuwa, anaishi vizuri, lakini kinachomchosha ni gubu la mume.

Salamu hizi ziko katika wimbo wa Vijana Jazz Band uitwao, 'Gubu la Mume', utunzi wake Hayati Hemed Maneti, uliorekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1980.

"Safiri salama kawasalimie wote na ukifika salama urudishe majibu mapema. Salamu sana kwa baba, salamu sana kwa mama, uwaeleze sijambo, bali nimekonda kwa gubu la mume. Hakuna kitu ninachokosa humu nyumbani, kama ni nguo ninavaa za kila aina, toka vitenge mpaka khanga hazinipiti, ila gubu tu la mume."

Ndugu yake anaahidi atazifikisha, lakini na yeye anampa nasaha zake ambazo zipo kwenye kiitikio cha wimbo huo na eneo la kuimbisha.

"Japokuwa ana gubu nakuomba vumilia, shemeji yangu kweli ana gubu, hawezi kuiacha tabia hiyo. Nakuomba uvumilie, hasira weka pembeni, kila mume na tabia yake, wengine ni walevi sana, wengine hupiga sana na wengine wana gubu sana, lakini wenzako huvumilia."

Bendi hiyo hiyo ya Vijana Jazz, katikati ya miaka ya 1980, iliingia studio na kurekodi wimbo uitwao 'Nilitaka Iwe Siri.'

Hiki ni kisa cha wanandoa wawili walioachana bila kuweka wazi ni kitu gani kimesababisha hilo.

Sasa mwanamume anapita mitaani na kumtangazia ubaya 'ex' wake sababu za uongo zilizofanya waachane. Kila akipita mtaani anakutana na tuhuma zake kuwa yeye ndiye chanzo cha kusambaratika kwa ndoa.

Jambo hilo likawa linamkereketa sana rohoni kwani yeye anajua ukweli wote na sababu ya kuachana na 'ex' wake.

Siku moja uzalendo ukamshinda naye akamua amwage mboga. Akaanika kila kitu ili ieleweke kwa sababu anatangaziwa sana ubaya mitaani. Akamkuta yuko na marafiki zake, akamfuata hapo hapo na kuanza kuyamwaga hadharani. Akawa anampasha mwenyewe huku pia anawaambia marafiki zake wasikilize sababu halisi ya wao kuachana kwa kuwa alikuwa mstaarabu kutotaka mambo yajulikane. Lakini kwa sababu anapakwa ubaya, basi bora tu afunguke.

Wimbo huu ulitungwa na Cosmas Thobias Chidumule.

"Niliitaka iwe siri yetu, mimi nawe. Sikutaka watu wafahamu kilichotutengenisha. Ewe Mtalaka wangu, mzazi mwenzangu eee, ukaanza kunitangaza vibaya, mimi mama ooo.

Nimevumilia leo nitasema yote, ieleweke. Nani wa kulaumiwa kati yetu mimi nawe, ooo mama ooo."

Baada ya hapo, akawageukia rafiki zake na kuwaambia sababu halisi ya kuachana na rafiki yao.

"Ninapokula ananisema, mama ooo, kwenu ulikuwa huli hivyo, kula unenepe mama, akinunua nguo ananisimanga, mama ooo, kwenu uliokuwa hujui kuvaa, vaa upendeze dada, nilijipondoa ananicheka, mama ooo, kwenu ulikuwa hupaki wanja, paka ujidai dada."

Wanawake saluti kwenu, mnavumilia mengi sana ila endeleeni kuvumilia. Ndoa ina tamu na chungu.

**Tuma meseji 0716 350534**

## HADITHI

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 14

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




INA maana kaka unashindwa kulitatua hili, unaniachia mimi kweli?" Havijawa akaanza kulia.

"Dada, mimi nimechoka kuishia hapa. Maneno kila siku wewe na wifi yako. Na kwa bahati mabaya hili limetokea, nimeamua kuondoka."

"Sasa wewe unaondokaje unaniacha mimi dada yako?"

"Nakwenda kuishi ukweni! Mke wangu ana baba yake mdogo kule Kibada. Ameshatuambia twende tukaishi kule, yeye haishi pale, ila ana nyumba ambayo ameimaliza, lakini haina mtu wa kuishi."

"Kaka wee, na mimi je nitaenda wapi?"

"Havijawa wewe ni mtu mzima sasa, haiwezekani tukafuatana kama watoto wadogo. Mimi nina mke, na wewe tafute sehemu ukaishi, ukapange hata chumba." Akajibu Kassim, halafu kama kuna mtu akakumbuka.

"Au nitamuuliza mke wangu kama tunaweza kwenda kuishi wote. Lakini sijui kama atakubali. Hivi mnavyoparurana, unafikiri atakubali?"

Havijawa hakusema kitu, akabaki analia na moyo wake.

*********************************

Ukweli ni kwamba kila kitu hakikuwa kweli. Hakukuwa na kiwanja feki wala kubomolewa nyumba.

Mpango huo ulifanywa na Kassim pamoja na rafiki yake mmoja aitwaye Pembe.

Kwa bahati nzuri, Havijawa alikuwa hajawahi kumuona rafiki huyo wa kaka yake, hivyo alivyokuja pale na kujifanya ni Ofisa kutoka Wizara ya Ardhi aliaminika.

Mkakati huu ulitengenezwa ili kuzima tabia mbaya ya havijawa ya kumnyanya wifi yake.

Mpaka hapo tayari Havijawa alishajua nyumba itabomolewa, yeye hatokuwa na pa kwenda. Hana mpenzi, hana mume. Hafanyi biashara yoyote. Hajishughulishi ya biashara yoyote ya kuweza kumuingizia kipato. Yeye kazi yake kubwa ni umbea tu, kufitinisha watu, pamoja na kumuonea wifi yake.

Aliona kama kaka yake akienda ukweni yeye hawezi kwenda. Anachokifanya kwa wifi yake si kitu ambacho kinaweza kumfanya kukubali wote waongozane wakaishi huko. Kwanza yeye mwenyewe ataanzaje kunyanyua mguu wake, kuongozana na wifi yake kwenda Kibada. Aliona hiyo itakuwa ni nafasi ya wifi yake kulipiza kisasi.

Siku ya tukio hilo la mpango wa Kassim na Pembe, Sauda hakuwepo. Alikwenda kwao Kondoa kwenye msiba wa ndugu yake.

**Kila mmoja mtaani akawa anajua jambo hilo. Na mashoga zake wote wakamwambia afanye kama alivyoambiwa na kaka yake kwa sababu kwanza kugombana si lazima, lakini pia hiyo ndiyo itakuwa ndiyo njia itakayosababisha nyumba isiuzwe wala kubomolewa.**

Walijua kabisa mpango huo utamchanganya Havijawa na kweli ilikuwa hivyo. Wakamuachia mwenyewe sasa kusuka au kunyoa.

Mkutano wa pili ukiwa ni watu wawili tu, Kassim na dada yake Havijawa. Safari hii Kassim alikuwa na wazo moja wauze nyumba halafu wagawane pesa nusu kwa nusu, kila mmoja aende anakokufahamu.

"Sasa nyumba si ina kesi hii kaka, itakuwaje?" "We hujui mambo ya mjini. Tunamuuzia yeye akiwa hajui, atakaa baadaye wakiwa watu wa ardhi sisi hatupo." "Mimi naona kama hili si zuri sana, haya tutauza, mimi nitapata pesa, zikiniishia nitakwenda wapi?"

"Sasa hebu niambie dada Havijawa tufanye nini, mimi naona hii njia ndiyo nzuri kwanza itawafanya wewe na wifi yako msiishi pamoja, maana kila kukicha nyinyi ugomvi tu. Kila mtu akiwa kwake itakuwa safi sana."

Suala hili liliendelea kumchanganya Havijawa. Hakuona kama anaweza kuendesha maisha yake vizuri huko mbele kama wakiuza nyumba ya baba yao ambayo tayari ina mgogoro.

"Mimi nakuomba kaka yangu, tupambane kwanza na kesi, tafuta mwanasheria tunaweza kushinda." Havijawa alimshauri kaka yake.

Kassim alitabasamu kwa sababu alijua dada yake tayari ameshajaa kwenye mfumo. "Mimi nimekubali. Nitatafuta mwanasheria mzuri wa kusimamia kesi yetu, lakini nina ombi moja, ukikubali hilo tu, nitatekeleza ulichosema."

"Lipi hilo kaka yangu?"

"Ni kwamba umuombe radhi wifi yako kwa yote ambayo umemfanyia. Sitaki kurudia, unayajua. Nataka kama kesi ikiisha wewe ukae hapa, na mke wangu akae hapa kwa uhuru, siyo tena maneno, mpaka mimi natukanwa na watu huko mitaani kuwa naacha mke ananyanyaswa na kusimangwa."

Kusikia hivyo, Havijawa kwanza alishtuka na kukaa vizuri, akaonekana kumsikiliza kwa makini kaka yake.

"Kama sivyo basi mimi wazo langu litakuwa ni lile lie. Kuuza nyumba ili tugawana pesa, kila mtu afe na chake, au kuacha ije kuvunjwa na mimi na mke wangu tutakwenda kuishi hata ukweni." "Sawa kaka mimi nimekuelewa nitafanya hivyo." Aliamuahidi kaka yake. Tangu habari ile ya nyumba yao kuwa na hati feki, ilimchanganya sana Havijawa.

Hakuwa na raha kama siku zote. Na kwa sababu yalikuwa yamemfika shingoni, akawa anahadithia watu mitaani. Kila mmoja mtaani akawa anajua jambo hilo. Na mashoga zake wote wakamwambia afanye kama alivyoambiwa na kaka yake kwa sababu kwanza kugombana si lazima, lakini pia hiyo ndiyo itakuwa ndiyo njia itakayosababisha nyumba isiuzwe wala kubomolewa.

Siku mbilui baadaye alimwita kaka yake na kumwambia amekubali suala hilo. "Kaka mimi hata leo niko radhi kumuomba msamaha wifi yangu, najua nimemuudhi na nimemkwaza sana, hata kwa simu mimi niko radhi."

"Hapana dada kwa simu haiwezekani, tusubiri arudi kutoka Kondoa tukae, umuombe rasmi."

"Sawa basi nipe simu hata niongee naye tu wifi yangu jamani." Ukarimu huo ulimshangaza hata Kassim mwenyewe aliyepanga mpango huo.

Akampigia simu mkewe na kuanza kuongea naye. Akaongea naye maneno machache, halafu akamshtukia kwa kumwambia.

"Ongea na wifi yako anataka kukusalimu."

"Wifi yangu gani?"

"Kwani una wifi wangapi, bwana hebu msalimie." Alisema akiwa anamkabidhi Havijawa simu.

"Habari za huko wifi." Akasalimia kwa upendo na bashasha, salamu ambayo si tu ilimshtua, pia ilimtisha Sauda.

"Nzu...nzuri, nani wi...wifi." Akajibu kwa kigugumizi.

"Ndiyo mimi wifi yako, nakusalimia, nilikuwa na kaka yangu hapa tunaongea, akakupigia simu, nikamwambia na mimi nipe nimsamilie wifi yangu, nimemkumbuka, utarudi lini?"

"Keshokutwa tunamaliza msiba, ukiisha tu narudi." Akajibu lakini akiwa na maswali mengi kichwani.

"Haya wifi yangu tutaongeza zaidi nikirudi." Akasema huku akimkabidhi kaka yake simu.

Dakika kumi baadaye, wakati Kassim akiwa ametoka nyumbani alisikia simu iliyokuwa mfukoni ikiita.

Akaingiza mkono mfukoni na kutoa simu yake. namba ilionyesha ni mkewe.

Alijua swali atakaloulizwa. Ambacho hakujua ni kwamba litaulizwa kwa vipi.

"Enhee imekuwaje, huyo ni Havijawa kweli aliyekuwa akiongea au mwingine?"

"Ni yeye."

"Huyu huyu ninayemjua mimi?"

"Hakuna mwingine mke wangu."

"Kimemsibu kipi tena?" Akauliza tena. "Na wewe naye usitake kujua sana. Ni kwamba wifi yako amebadilika na anataka ukija huku akuombe msamaha." "Aniombe msamaha mimi?"

"Ndiyo wewe."

"He, makubwa! Unajua mnanitisha mimi, kuna nini huko kimetokea mpaka kabadilika ghafla tu. Au mna mipango yenu mtu na dada yake?"

"Hapana, ukija nitakupa kukupa mchapo nini kimembadilisha."

"Hebu nidokeze, wewe si mume wangu, utaninyimaje ubuyu?"

"Mke wangu, subira siku zote yavuta heri, hapa nilipo kuna watu kibao, wakisikia si vizuri. Ila kwa kifupi amebadilika. Kilichombadilisha nini. Ukija nitakwambia. Najua yeye hatokwambia, lakini mimi nitakupa hiyo habari. Na ukija sasa ujue unakuja kama kuanza ukurasa mpya wa maisha. Siyo yake tena."

**INAENDELEA JUMAPILI**



# HENNESSEYY, ELLA DA BWAY WAIKAZIA 'ANGUSHA'

STAA wa Bongo Fleva, Hennesseyy, ameendeleza ubabe kwenye muziki huo baada ya kutambulisha ngoma yake mpya 'Angusha' akimshirikisha Elly Da Bway.

Hennesseyy ambaye ni bosi wa lebo ya Spacious Music na Spacious Films, amejizolea umaarufu mkubwa kwa muziki wake ulioambatana na video zenye ubunifu.

Akizungumza hivi karibuni, Hennesseyy ameweka wazi kuwa miongoni mwa ngoma hiyo kali imetumia pesa nyingi kuiandaa.

"Maisha ya bata ndio maisha yetu halisi kwa hiyo tunachokionyesha kwenye video ndio kile tunachoishi kama Spacious Music, nashukuru kwa mapokezi mazuri ya Angusha, yametufanya tumeendelea kukaza kwa kutoa video za gharama,"amesema.

# IRENE KUIPA 'FARAJA' DUNIA



MWIMBAJI anayekuja kwa kasi katika muziki wa Injili, Irene Falifali, amewataka mashabiki kukaa tayari kupokea wimbo wake mpya, unaoitwa 'Faraja' ambao utatambulishwa hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe, Irene ambaye huduma zake anafanyia mkoani Morogoro amesema kwamba ameamua kutunga kibao hicho kutokana na mioyo ya watu wengi kupondeka kwa ugumu wa maisha, hivyo kwa kutumia wimbo huo utawafariji na kuwatia moyo.

"Tunapitia changamoto nyingi ikiwamo kukataliwa na kudharauliwa, wapo wanaokuambia hautaweza au umeshachelewa, lakini ninachojua mimi wakati wa Mungu ndio sahihi na ukifika hakuna anayeweza kuzuia," amesema Irene.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NETO ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imebadili uwezekano wa kumsajili, Pedro Neto kutoka Wolves msimu huu, kwa dau la takriban pauni milioni 60 inayodhaniwa inatosha kumnasa winga huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 23 ingawa Liverpool pia wanamtaka. ***(Mail)***

### SON, SPURS KITAELEWEKA

TOTTENHAM Hotspur imeanza mazungumzo na nahodha, Son Heung-min kuhusu mkataba mpya na wana imani makubaliano na mshambuliaji huyo wa Korea Kusini mwenye umri wa miaka 31 yatakamilika msimu huu. ***(Football Insider)***

### SOLANKE ATAKIWA WEST HAM

KOCHA wa West Ham, David Moyes, amezungumza na wanafamilia wa mshambuliaji wa Bournemouth, Dominic Solanke, mwenye umri wa miaka 26 kuhusu uwezekano wa kumsajili kwa ajili ya msimu ujao. ***(Football Transfers)***

### WAARABU WAMTAKA BRUYNE

KLABU za Ligi Kuu ya Saudi Arabia zimejiandaa kutoa zaidi ya pauni milioni 100 kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Kevin De Bruyne, mwenye umri wa miaka 32, kutoka Manchester City. ***(Football Insider)***

### NETZ AGOMBEWA ENGLAND

ARSENAL, Manchester United, Newcastle United na Chelsea zote zimeonyesha nia ya kumnunua beki wa kushoto wa Borussia Monchengladbach, Luca Netz, mwenye umri wa miaka 20. ***(HITC)***

### ZEBRI AINGIA SOKONI

BAYERN Munich imemwongeza Kocha wa Brighton, Roberto de Zerbi, katika orodha fupi ya warithi wanaotarajiwa kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel mwishoni mwa msimu huu, lakini mwalimu wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, ambaye pia anasakwa na Liverpool, anabakia kuwa chaguo la kwanza la klabu hiyo. ***(Mirror)***

### WILLIAM ATAJWA CHELSEA

CHELSEA ni moja ya klabu mbalimbali zinazomfuatilia winga wa Athletic Bilbao, Nico Williams, mwenye umri wa miaka 21. ***(ESPN)***

### EDWARDS KUTUA LIVERPOOL

MICHAEL Edwards anakaribia kukubaliana juu ya nafasi ya juu na wamiliki wa Liverpool, Fenway Sports Group, ambayo itajumuisha mtendaji mkuu wa zamani wa Wekundu hao kuchukua udhibiti wa shughuli za soka za klabu. ***(Athletic)***

### CHELSEA, ROMA MAMBO SAFI

CHELSEA ipo tayari kukubali ofa kutoka kwa AS Roma kwa ajili ya Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, ambayo ni chini ya chaguo la pauni milioni 37 la kununua lililojumuishwa katika mkataba wa mkopo wa mshambuliaji huyo wa Ubelgiji. ***(Calcio Mercato, via Team Talk)***

### ROWE KUTUA WEST HAM

WEST Ham inaweza kumlenga kiungo wa kati wa Arsenal, Emile Smith Rowe, mwenye umri wa miaka 23 katika dirisha la usajili. ***(Caught Offside)***

### ARSENAL YAMTAKA MENDES

ARSENAL inamfuatilia beki wa Brazil, Douglas Mendes, mwenye umri wa miaka 19, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Red Bull Bragantino akitokea Red Bull Salzburg. ***(Football Transfers)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA YAJIPANGA KUMBAKISHA FELIX

**Ni baada ya nyota huyo kuonyesha nia ya kubakia Katalunya ingawa...**

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA iko mbioni kumsajili, Joao Felix, kwa mkopo kutoka Atletico Madrid kwa msimu mwingine, kwa mujibu wa ripoti kutoka Hispania.

Felix alitua Barcelona siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho wa majira ya joto mwaka jana, akijiunga na La Blaugrana hao kwa mkopo hadi mwisho wa msimu. Mpango huu haukujumuisha kifungu cha ununuzi cha hiari au cha lazima.

Kwa mujibu wa ripoti ya Sports, Wakala wa Felix, Jorge Mendes, amemjulisha Rais wa Barcelona, Joan Laporta, kuhusu mazungumzo na Atletico ya mkopo mwingine yanaendelea vizuri.

Barca wako tayari kumbakisha Felix ikiwa hali ya kifedha ni sawa kwao na wamepokea uhakikisho itakuwa hivyo.

Atletico walikuwa na matumaini ya kumuuza Felix au kuambatanisha kipengele cha ununuzi chenye thamani ya euro milioni 75 kwa mkopo mwingine kufuatia mwanzo wake mzuri wa maisha ndani ya Barcelona, lakini kiwango chake kimeshuka katika miezi ya hivi karibuni na itakuwa vigumu kumbadilisha mara moja.

Barca hawataki kukubaliana na kifungu cha ununuzi chenye thamani ya zaidi ya euro milioni 40 kwa Felix.

Baada ya kutofautiana na Kocha, Diego Simeone, Atletico wameweka wazi Felix hataichezea tena, jambo ambalo linaweza kuwaweka pabaya katika mazungumzo ya kumbadilisha.

Barcelona hawana nia ya kumsajili moja kwa moja Felix msimu huu wa joto kutokana na kushuka kwa kiwango chake. Fowadi huyo wa Ureno anaweza kupokea ofa kutoka Saudi Aarabia msimu huu wa joto, lakini anapendelea kubakia Katalunya.

Felix pia ana matumaini anaweza kumvutia kocha wa mpya wa Barcelona, huku bosi wa sasa Xavi akiondoka mwishoni mwa msimu.

Xavi hakumwona Felix kama usajili wa kipaumbele lakini klabu imedhamiria kumbakisha bila kujali.

Matumaini ya Barcelona ni Felix kusalia kwa mkopo kwa msimu mwingine na wanaweza kumsajili kwa mkataba wa bei nafuu mwaka 2025.

# MADRID YAGOMEA DAU LA DAVIES

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid haiko tayari kulipa zaidi ya euro milioni 40 ili kumsajili Alphonso Davies kutoka Bayern Munich msimu huu wa joto, kwa mujibu wa ESPN.

Davies ameibuka mmoja wa wachezaji wawili wanaolengwa na Madrid katika dirisha la majira ya joto pamoja na Mfaransa, Kylian Mbappe wa Paris Saint-Germain.

Tofauti na Mbappe, ambaye mkataba wake umemalizika na hatahitaji ada ya uhamisho ili kusaini lakini badala yake anadai mkataba mnono, Madrid italazimika kulipa ada ya uhamisho ili kumleta Davies.

Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada kwenye Uwanja wa Allianz Arena unaendelea hadi mwakani na ripoti kutoka Madrid zimedai wamemtaka nyota huyo asisaini mkataba mpya ili waweze kurahisisha uhamisho wake kwa urahisi zaidi.

Kwa mujibu wa ESPN, Madrid wanasita kwenda zaidi ya hesabu yao ya euro milioni 40 kwa Davies kutokana na hali ya mkataba wake hiyo ni tofauti na bei iliyowekwa na Bayern Munich kumnasa nyota huyo ambayo ni euro milioni 60.

Hatimaye Bayern Munich hawataki kutimiza matakwa ya Davies ya mshahara wa jumla wa thamani ya euro milioni 20 kwa mwaka, wakati Madrid hawana matatizo kama hayo kulipa kiasi hicho.

Idadi hii inasimama karibu mara mbili ya kiasi ambacho Los Blancos wanamlipa David Alaba, ambaye alijiunga nao kutoka Bayern kwa uhamisho wa bure mnamo 2021.

Sakata la Davies limelinganishwa na lile lililohusisha Madrid na Bayern kuhusu uhamisho wa Toni Kroos mwaka 2014, kiungo huyo akibadilishana na Ujerumani kwenda Hispania kwa dili la thamani ya euro milioni 25 baada ya kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake.

Katika nafasi ya Davies, Bayern Munich wanataka kumsajili beki wa kushoto wa AC Milan, Theo Hernandez, ambaye wakati mmoja alikuwa kwenye vitabu vya Madrid.




# Klopp amsifu Guardiola wakikutana

**LONDON, England**

VINARA wa Ligi Kuu England, Liverpool wanawakaribisha mabingwa watetezi Manchester City leo huku pande zote zikifuatilia historia katika mpambano mkubwa kujiimarisha kileleni.

Huku tayari wakiwa wametwaa Kombe la Carabao, Liverpool wanatafuta mataji manne, wakati Manchester City inaweza kuwa timu ya kwanza kushinda mataji matatu mfululizo.

Inaweza pia kuwa mechi ya mwisho ya Ligi Kuu England kati ya Jurgen Klopp na Pep Guardiola.

„Nafanya kazi mwenyewe hivyo naona ubora ninapokabiliana nao na Pep ni hivyo," alisema Klopp.

Liverpool na City wameshinda kila taji England tangu mwaka 2018, huku timu ya Klopp ikimaliza kileleni mwaka 2020 na Guardiola mshindi mara tano.

„Jinsi ambavyo amekuwa na ushawishi katika soka, kushinda kiasi cha mataji aliyoshinda katika maisha yake ya soka ni jambo la kawaida," aliongeza Klopp.

„Lakini ukimwona kwenye mstari anafanya kama hajawahi kushinda hapo awali. Nia aliyonayo ni bora kabisa.

„Katika maisha yangu yeye ndiye kocha bora, bila shaka."

Ingawa Guardiola na Klopp ni maadui wanaofahamika, wawili hao hawajapata nafasi nyingi za kukutana ugenini.

Timu sita za juu kwenye jedwali la Ligi Kuu England, Liverpool wakiwa kileleni kwa pointi 63, Manchester City 62, Arsenal 61, Aston Villa 55, Tottenham 50 na Manchester United 44.



Liverpool wanakwenda katika mchezo wa leo wakiwa na pointi moja pekee mbele ya City na wakiwa na tofauti kubwa ya mabao.

Lakini kuna mvutano wa pande tatu za kuwania taji hilo msimu huu Arsenal wakijikuta wakiwa kwenye vita baada ya kuanza kwa mwaka vibaya.

Kikosi cha Mikel Arteta kimeshinda mechi zao saba za mwisho za ligi na kukaa pointi mbili pekee nyuma ya Liverpool na kuwa na tofauti kubwa ya mabao kwa pande zote mbili.

Liverpool wana rekodi nzuri dhidi ya Manchester City katika uwanja wa Anfield, wakipoteza mara moja tu wakiwa nyumbani tangu 2003 na kushinda mechi 13 kati ya 20 zilizopita.

## Chelsea mtegoni ikiivaa Newcastle

**LONDON, England**

CHELSEA imethibitisha beki wa kushoto, Ben Chilwell, ataonana na daktari baada ya kupata jeraha jipya la goti, huku The Blues wakiwa na majeruhi kadhaa kabla ya kukutana na Newcastle United hapo kesho.

Chilwell, ambaye alirejea kutoka nje ya uwanja kwa miezi mitatu kutokana na jeraha la msuli wa paja mnamo Januari, alicheza dakika zote 90 dhidi ya Brentford mara ya mwisho lakini alipata tatizo la goti wakati wa mechi ambalo limemfanya ashindwe kufanya mazoezi tangu wakati huo.

„Tunahitaji kusubiri hadi atakapoonana na mtaalamu," Kocha Mkuu, Mauricio Pochettino, alisema akiwaambia waandishi wa habari kuhusu beki huyo wa kushoto.

„Siwezi kwenda mapema. Natumaini sio suala kubwa lakini kwa wakati huu baada ya miezi nane au tisa na klabu, napendelea kuwa waangalifu na kusubiri."

Beki wa kati, Levi Colwill, pia alipata tatizo la vidole vya mguu dhidi ya Brentford ambalo limemfanya ashindwe kufanya mazoezi, huku kiungo Conor Gallagher akiwa hajisikii vizuri na amekosa mazoezi pia.

Kuhusu Gallagher, Pochettino alieleza: „Bado hayupo. Katika siku tatu za mwisho za mazoezi, hayupo. Tutaona kama anaweza kuwa na uwezekano wa kufanya mazoezi.

"Tatizo la hali ya aina hii unapungua uzito, nguvu huwa chini, unahitaji muda wa kupona na kuona kama inawezekana kupatikana na kupatikana kwa kiwango gani, tunatakiwa kumtathmini katika siku chache zijazo."

Pochettino alikiri kuchanganyikiwa kwake kwa kile anachohisi ni „bahati mbaya" kwenye eneo la mbele la majeruhi, akifichua kuwa hajawahi kukumbana na mdudu mkubwa wa jeraha hapo awali.

„Tunakumbuka mambo ya zamani tukiwa na klabu tofauti, nadhani hii ndiyo bahati mbaya zaidi ya maisha yake," aliongeza Pochettino.

„Tayari tulipofika Chelsea, tulichambua hali hiyo, hiyo ilikuwa moja ya pointi dhaifu zaidi katika msimu uliopita, majeraha mengi. Bahati mbaya sana, unajua?

„Wakati mwingine, bahati mbaya au bahati nzuri, sipendi kuzungumza kwa njia hii kwa sababu inaonekana kama unafanya kazi au hufanyi kazi vizuri, unahitaji kuwa na bahati nzuri au mbaya. Lakini nadhani ni mambo mengi sana."

HABARI MICHEZO

# HATIMA SAKATA LA DUBE J'TANO, ATAJWA YANGA

Na Saada Akida

UONGOZI wa Azam FC umesema utatoa msimamo wake kuhusu uamuzi wa mshambuliaji wake, Prince Dube, aliyeandika barua ya kutaka kuondoka klabuni hapo ifikapo Jumatano, imeelezwa.

Hata hivyo taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanatajwa kumwinda mshambuliaji huyo ambaye amekuwa na kiwango bora kila anapokutana na vigogo wa soka nchini.

„Kuna taarifa Yanga imeanza mchakato wa ndani wa kumwania Dube, naona ni vita nyingine na jeuri ya fedha tutaishuhudia katika usajili hapa nchini," kilisema chanzo chetu.

Machi 4, mwaka huu, Dube, raia wa Zimbabwe aliiandikia barua Azam akiomba kuvunja mkataba wake kutokana na kutaka kujiunga na klabu nyingine ili kufikia malengo yake.

Klabu hiyo yenye makao yake Chamazi, Dar es Salaam ilimjibu mshambuliaji huyo iko tayari kuvunja mkataba walioingia endapo watalipwa kiasi cha Dola za Marekani 300,000, ambacho kimeandikwa kwenye makubaliano.


Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam, Zakaria Thabit, 'Zaka', alisema klabu hiyo imepanga kutangaza uamuzi wake rasmi Jumatano baada ya kukaa kimya huku mshambuliaji huyo akiendelea kushikilia msimamo wake wa kutaka kuondoka.

Zaka alisema wanatambua Dube bado ni mchezaji wao halali kama mkataba unavyosema na hawana hofu yoyote juu ya uamuzi aliouchukua.

"Kwa sasa tumeamua kukaa kimya lakini ikifika Machi 13, mwaka huu, itakuwa siku ya Jumatano tutazungumza na kuweka wazi juu ya hatima ya Dube na sisi Azam FC," alisema Zaka.

Dube pia katika barua yake aliyoandika amewashukuru wafanyakazi na mashabiki wote wa Azam FC kwa safari yao ya miaka minne waliyokuwa pamoja.

Mshambuliaji huyo pia amekaririwa akisema anataka kujiunga na timu yenye malengo ya kutwaa ubingwa na anaiona Azam FC ni klabu isiyokuwa na ndoto hiyo huku akishanganzwa na viongozi wa klabu hiyo wakiwa na ‚mapenzi' na Simba na Yanga.



Rais wa Yanga, Hersi Said (kushoto), akiwa ameenda kumtembelea kiungo wa timu hiyo, Khalid Aucho, ambaye amefanyiwa operesheni ndogo ya goti jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

# Biashara United yakwama Mbeya

Na Adam Fungamwango

MATUMAINI ya Biashara United FC kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi ya Championship yamefifia baada ya kukubali kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City katika mechi kati ya raundi ya 24 ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini, Mbeya juzi.

Mbeya City ilikuwa ya kwanza kupata bao dakika ya 11 likiwekwa wavuni na Maulid Shaaban na Boban Zirintusa aliisawazisha kwa upande wa Biashara United dakika ya 45.

Biashara United yenye pointi 50 ilikuwa inahitaji ushindi huo kwa udi na uvumba ili kuifukuza KenGold ambayo ipo kileleni katika msimamo wa Ligi ya Championship ikiwa na pointi 53. Sare hiyo inahatarisha nafasi ya ya pili ambayo pia inawaniwa na Pamba FC iliyoko nyuma kwa tofauti ya pointi mbili huku ikiwa na mchezo mmoja mkononi.

Mechi nyingine ya ligi hiyo ilichezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha ambapo wenyeji TMA waliisulubu Transit Camp mabao 2-0 na kufikisha pointi 45 wakati kwenye Uwanja wa Nyamagana, Copco ilitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Mbeya Kwanza.

Matokeo ya mechi hiyo yanaifanya Mbeya Kwanza kupaa hadi nafasi ya nne ya msimamo ikiwa na pointi 47 na Copco ikibakia katika hali mbaya ikiwa na pointi 18.

Timu mbili zitakazomaliza katika nafasi ya juu zitapanda daraja moja kwa moja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

## Mlandege yatakata, Kipanga 'OUT' FA

NA Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WANAJESHI wa Kipanga wameondolewa katika mashindano ya Kombe la FA Zanzibar baada ya kuchapwa mabao 2-0 na Black Sailor inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza katika mechi ya michuano hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ngome ulioko Fuoni juzi.

Akizungumzia na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Kipanga, Hassan Abdulrahman, alisema kuondolewa mapema katika mashindano hayo kumeharibu mipango yao waliyojiwekea katika msimu huu.

Kocha huyo alisema baada ya mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kuwa mgumu kwao, walielekeza nguvu zao katika mashindano hayo lakini sasa anaona pia hawakuwa na bahati ya kufanya vizuri kwa kuruhusu kufungwa.

Alisema awali mpango wao namba moja ulikuwa ni kutwaa taji la Ligi Kuu Zanzibar lakini baada ya kuona mipango hiyo haiwezekani, waliongeza nguvu katika Kombe la FA na matokeo ya kufungwa yamewaumiza.

"Tulishiriki mashindano hayo kwa sababu malengo yetu makubwa yalikuwa ni kuhakikisha tunatwaa ubingwa wa michuano hii, lakini lengo letu halikutimia, tumehuzunika, tunasema haikuwa bahati kwetu," alisema Abdulrahman.

Aliongeza baada ya kuondolewa katika mashindano hayo ya FA, sasa wanaelekeza nguvu katika michezo 10 ya Ligi Kuu Zanzibar iliyosalia ili kuhakikisha wanamaliza msimu wakiwa katika nafasi nne za juu.

"Tumeshindwa kulibeba Kombe la FA, lakini sasa inabidi turudi mchezoni katika Ligi Kuu Zanzibar, tunamichezo 10 ambayo tukicheza vizuri na kuchanga karata zetu vyema, tukijiimarisha katika kila mipango basi tutamaliza ligi hiyo katika nafasi nzuri," aliongeza kocha huyo.

Timu nyingine zilizoondolewa katika mashindano hayo ni Villa FC ambayo ilifungwa penati 5-3 na Kilimani City baada ya kumaliza dakika 90 wakiwa na sare ya bao 1-1.

Mlandege FC ilisonga mbele baada ya kuipa kichapo cha mabao 6-2 Eleven Star wakati leo Black Lion watawavaa Paje Star FC kwenye Uwanja wa Kitogani huku Uhamiaji ikikutana na Ujamaa kuanzia saa 8:00 mchana kwenye Uwanja wa Mau A na jioni kwenye uwanja huo huo Zimamoto itacheza dhidi ya Shangani FC wakati Kundemba yenyewe itapambana na Maafande wa Polisi FC.

**Barcelona yajipanga kumbakisha Felix** UKURASA 21



# Michezo

Jumapili Machi 10, 2024
Nipashe



Mshambuliaji wa Simba, Willy Essomba Onana (kulia), akijiandaa kumtoka nyota wa Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga jana. Simba ilishinda mabao 2-1. **PICHA: SIMBA SC**

# ONANA AIBEBA SIMBA

## ●●● Bao lake larejesha furaha Msimbazi, Jamhuri Moro ikifungiwa...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la winga Mcameroon, Willy Onana ambaye alifunga muda mfupi tu baada ya kuingia liliipa Simba ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani, jijini Tanga jana.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea Rayon FC ya Rwanda, alipata mpira nje kidogo ya eneo la 18, akaumiliki na kuingia nao ndani ya eneo la hatari akiruka viunzi vya wachezaji wa Coastal Union kabla ya kuukwamisha wavuni kwa umaridadi, akimwacha kipa Mkongomani Ley Matampi na mabeki wake wakiruka kuuzuia bila mafanikio.

Mpira huo ulianza kwa kwenda kugonga nguzo ya pembeni chini kabla ya kujaa wavuni, dakika ya 72 ya mchezo huo.

Ni bao lake la pili katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, la kwanza akilifunga katika mechi ya ufunguzi, Agosti 17, mwaka jana dhidi ya Mtibwa Sugar, mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani, Morogoro, Simba iliposhinda mabao 4-2.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa mchezaji huyo baada ya kuwa nje kwa muda kutokana na majeruhi, akiuguza nyama za paja.

Bao hilo lililosimama dakika 90 za mchezo, limeleta furaha na ahueni kwa wanachama na mashabiki wa Simba kwani Jumatano waliambulia kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Maafande wa Tanzania Prisons.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kufikisha pointi 39, saba nyuma ya vinara wa ligi hiyo na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 46, timu zote zikiwa zimecheza michezo 17 lakini yanaibakisha Coastal Union kwenye nafasi ya nne, ikiwa na pointi 27, ikiwa imeshacheza michezo 20.

Dakika nne za kwanza, mpira ulichezwa bila timu yoyote kufika katika lango la mpinzani na dakika iliyofuata Coastal Union walibisha hodi kwenye lango la wageni wao kwa kumjaribu kipa raia wa Morocco, Ayoub Lakred, kupitia kwa straika wao tegemeo Mghana, Denis Modzaka.

Akiwa ndani ya eneo la hatari, huku mabeki wa Simba wakiwa wamezubaa kumkaka, Modzaka aliachia shuti kali la juu, lakini Lakred alifanikiwa kuruka na kuupiga ngumi mpira na kuwa kona.

Simba ilifanikiwa kupata bao la kuongoza dakika ya 11 ya mchezo, likiwekwa na Freddy Michael, aliyeunganisha moja kwa moja kona iliyopigwa na Clatous Chama.

Raia huyo wa Ivory Coast akiwa katikati ya walinzi, aliunganisha mpira kwa mguu wa kulia na kwenda pembeni ambapo licha ya juhudi za kipa wa Coastal Union, Matampi kuruka kutaka kuupangua hazikufanikiwa.

Kwa Freddy, pia ni bao lake la pili kufunga msimu huu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, moja akilipata katika mechi dhidi ya Tabora United lakini Modzaka alifanya tena jaribio kama la mwanzo, alipowatoka mabeki wa Simba na kupiga shuti kali, nje kidogo tu ya eneo la hatari, lakini safari hii mpira ulipaa juu.

Bao hilo lilifungwa na Lucas Kikoti dakika ya 24 ya mchezo, baada ya kupokea kona fupi kutoka kwa Miraji Hassan ambapo ilionekana kama atapiga krosi, lakini alipiga mpira moja kwa moja, ukaenda kujaa wavini licha ya jitihada kubwa kutoka kwa Lakred ya kutaka kuuokoa.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko ambapo Simba iliwatoa, Freddy, Babakar Sarr, Luis Miquissone na Saido Ntibazonkiza na nafasi zao zilichukuliwa na Pa Omari Jobe, Kibu Denis, Mzamiru Yassin na Onana, huku Coastal Union ikiwapumzisha Kikoti, Modzaka na Jackson Shiga, nafasi zao zikajazwa na Paul Kisindi, Bakari Selemani na straika anayecheza kwa mkopo akitokea Yanga, Crispin Ngushi.

Wakati huo huo, Simba inarejea kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam baada ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), kuufungia Uwanja wa Jamhuri, Morogoro.

# Yanga : Harufu ya ubingwa inanukia

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya wenyeji Namungo FC, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema sasa ameanza kuona matumaini ya timu yake kutetea taji la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Yanga imerejea tena kileleni baada ya kufikisha pointi 46 wakiwa wamecheza michezo 17 huku nafasi ya pili ikishikiliwa na Azam FC yenye pointi 44, lakini imeshuka dimbani mara 20.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gamondi, alisema ameridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mechi hiyo na kuwataka waendelee kupambana zaidi kwa sababu wana nafasi kubwa katika mbio za kutwaa ubingwa.

Gamondi alisema alizungumza na nyota wake kabla ya mchezo na kuwaambia kama wanahitaji ushindi wanapaswa kucheza kikubwa na kwa malengo jambo ambalo walifanikiwa kulifanya na hatimaye kuvuna pointi tatu muhimu.

"Tunachohitaji ni kushinda kila mchezo ili kutetea ubingwa, mapema nilizungumzia hilo lakini ushindi ndio silaha pekee itakayotupa tunachohitaji, kwa sasa tunaenda hatua kwa hatua kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Gamondi.

Aliongeza katika kipindi cha kwanza katika mchezo huo nyota wake walipoteza nafasi lakini baada ya kupumzika walilazimika kuongeza juhudi na kufanikiwa kupata mabao.

Naye kiungo wa timu hiyo, Mudathir Yahya, alisema walihitaji pointi tatu sana, na kuweka wazi kipindi cha kwanza kilikuwa kigumu kwao lakini walipambana na kujituma ili kuondoka na alama tatu muhimu na kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo.

"Hii mechi tulihitaji pointi tatu, kocha alituambia lazima tupambane na kujituma ili kuvuna alama hizo, tucheze kikubwa na hili limefanikiwa, suala la bingwa bado ligi inaendelea na bado tunaviporo, tunatakiwa kushinda," alisema Mudathir.

Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Shadrack Nsajigwa, alisema walianza vizuri mchezo huo lakini wapinzani wao walibadilika kwa kuongeza kasi na kutumia makosa ambayo waliyafanya.

Nsajigwa alisema Yanga ilitumia ,ukubwa' na uzoefu na ndio sababu ya wao kupoteza mechi hiyo licha ya kujaribu kuwazuia lakini haikuwa rahisi kufanya hivyo muda wote.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >